

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**



**BUNGE LA TANZANIA**

**TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE  
YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KWA KIPINDI CHA MWAKA  
MMOJA KUANZIA JANUARI, 2016 HADI JANUARI, 2017**

Ofisi ya Bunge,  
S. L. P 941,  
**DODOMA**

Februari, 2017.

## YALIYOMO

SEHEMU YA KWANZA.....	1
1.0 MAELEZO YA JUMLA.....	1
1.1 Utangulizi .....	1
1.2 Majukumu ya Kamati .....	2
1.3 Njia na Mbinu mbalimbali zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati .....	4
1.4 Shughuli zilizofanyika .....	5
SEHEMU YA PILI.....	9
2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI .....	9
2.1 Maelezo ya Jumla .....	9
2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati.....	11
SEHEMU YA TATU .....	28
3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO .....	28
3.1 Maoni.....	28
3.2 Mapendekezo .....	31
SEHEMU YA NNE.....	37
4.0 HITIMISHO .....	37
4.1 Shukurani .....	37
4.2 Hoja.....	38



## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 MAELEZO YA JUMLA

#### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee na kuikubali Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kipindi cha Januari 2016 hadi Januari 2017.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii ya Mwaka inawasilishwa kwa mara ya kwanza tangu kuundwa kwa Kamati hii mwezi Januari 2016, ambapo uliteuwa Wajumbe ishirini na tatu (23). Kwa sasa Kamati ina Wajumbe 27 na naomba kuwataja kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb- Mwenyekiti
2. Mhe. Kanal (Mst) Masoud Ali Khamis, Mb- M/Mwenyekiti
3. Mhe. Capt (Mst) George Huruma Mkuchika, Mb- Mjumbe
4. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb- "
5. Mhe. Prosper J. Mbena, Mb- "
6. Mhe. Victor Kilasile Mwambalawa, Mb- "
7. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Mb- "
8. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb- "
9. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb- "
10. Mhe. Alphaxad Kangi Lugola, Mb- "
11. Mhe. Cosato David Chumi, Mb- "
12. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb- "
13. Mhe. Bonnah Kaluwa, Mb- "
14. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb- "
15. Mhe. Kiswaga Boniventura Destery, Mb- "

- |     |                                      |   |
|-----|--------------------------------------|---|
| 16. | Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb-         | " |
| 17. | Mhe. Joel Mwaka Makanyaga, Mb-       | " |
| 18. | Mhe. Haji Khatib Kai, Mb-            | " |
| 19. | Mhe. Lucy Simon Magereli, Mb-        | " |
| 20. | Mhe. Masoud Abdalla Salim, Mb-       | " |
| 21. | Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb-   | " |
| 22. | Mhe. Lazaro S. Nyalandu, Mb-         | " |
| 23. | Mhe. Stephen J. Masele, Mb-          | " |
| 24. | Mhe. Machano Othman Said, Mb         | " |
| 25. | Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb- | " |
| 26. | Mhe. Khamis Yahya Machano, Mb-       | " |
| 27. | Mhe. Yahya Omari Masare, Mb-         | " |

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa dhati kwa kuzingatia vigezo muhimu vilivyoainishwa katika fasili ya 5 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 na kuteuwa Wajumbe wenye Taaluma, Uzoefu na sifa nyingine muhimu kwa utekelezaji wa majukumu ya Kamati hii.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne zifuatazo:-

- i. Sehemu ya Kwanza ambayo inatoa maelezo ya jumla;
- ii. Sehemu ya Pili inayohusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati;
- iii. Sehemu ya Tatu ambayo inabainisha maoni na mapendekezo ya Kamati; na
- iv. Sehemu ya Nne ambayo ni hitimisho la taarifa hii.

## 1.2 Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane, Fasili ya 6, Kifungu cha 3 pamoja na Fasili ya 7, Kifungu cha (1) ya Kanuni za Kudumu za

Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ni moja kati ya Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta inayosimamia Wizara tatu ambazo ni Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Majukumu ya Kamati hii ni kama yafuatayo:-

- i. Kushughulikia Bajeti za Wizara inazosisimamia;
- ii. Kushughulikia Miswada na Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazosisimamia;
- iii. Kushughulikia taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na
- iv. Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na majukumu ya kusimamia Wizara, Kamati ina majukumu mengine matano (5) yaliyoainishwa kwenye Fasili ya 7, Kifungu cha 2, ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Majukumu hayo ni:-

- i. Kuimarisha ushirikiano kati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mabunge ya nchi nyingine;
- ii. Kufuatilia mwenendo na hali ya mtangamano wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika;
- iii. Kushughulikia taarifa za wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika;
- iv. Kushughulikia taarifa zote za wawakilishi katika Vyama mbalimbali vya kibunge ambapo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwananchama; na
- v. Kushughulikia Taarifa za hali ya Ulinzi na Usalama wa Mipaka ya Nchi na Usalama wa Raia na Mali zao.

**Mheshimiwa Spika**, mbali na majukumu ya msingi ambayo yameorodheshwa hapo juu, Kanuni ya 119 ya Kanuni za Kudumu za

Bunge imetoa rufusa kwa Kamati yoyote ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kupendekeza kwa Spika majukumu mengine ya nyongeza. Majukumu hayo ya nyongeza kwa mujibu wa Kanuni ya 119 yanatekelezwa kwa namna mbili zifuatazo:-

- a) Kamati kupendekeza ipewe jukumu la nyongeza; na
- b) Mheshimiwa Spika kukabidhi Kamati jambo lingine lolote kadri atakavyoona inafaa kwa ajili ya kufanyiwa kazi na Kamati hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki kinachotolewa taarifa hii, Kamati haikuwa na jukumu lolote la nyongeza kama ilivyoanishwa kwenye Kanuni ya 119.

### **1.3 Njia na Mbinu mbalimbali zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Kamati ilitumia njia na mbinu mbalimbali zilizoendana na matakwa ya Kanuni ya 117 (3) na (5) kuhusu kukutana na kuzingatia bajeti ya Kamati iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2015/2016 na 2016/2017. Njia zilizotumika ni:-

- i. Vikao na Wizara kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji za Wizara hizo pamoja na Taasisi zake;
- ii. Vikao na wawakilishi wa Vyama mbalimbali vya Kibunge kwa ajili ya kupokea na kujadili utekelezaji wa majukumu yao;
- iii. Kuwataka Mawaziri wafafanue na kutoa maelezo kuhusu masuala mbalimbali yaliyohitaji ufafanuzi;
- iv. Ziara za kujiridhisha na ufanisi wa utekelezaji wa masuala mbalimbali hususan Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati;
- v. Kuwasilisha kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti hoja mahsus zilizotokana na Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati za Mwaka wa Fedha wa 2016/2017; na

- vi. Kubadilishana mawazo na uzoefu na Kamati zinazosimamia Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama za Mabunge ya nchi nyingine.

#### **1.4 Shughuli zilizofanyika**

**Mheshimiwa Spika**, mara baada ya kuteuliwa, Wajumbe wa Kamati walifanya uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kwa mujibu wa Kanuni ya 116 (10) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016. Katika kipindi cha Januari, 2016 - Januari, 2017 Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama imetekeleza shughuli zifuatazo:-

##### **1.4.1 Mafunzo kwa Wajumbe kuhusu Kazi na Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia kuwa Wajumbe wa Kamati ni wapya, walipatiwa mafunzo kuhusu Kazi na Majukumu ya Kamati, ili waweze kufahamu kazi na majukumu ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Mafunzo hayo yalitolewa tarehe 21 Januari, 2016.

Aidha, baada ya kupokea mafunzo hayo, tarehe 23 Januari, 2016 Wajumbe waliandaa Mpango Kazi wa Kamati kwa kipindi cha Januari

- Juni 2016.

##### **1.4.2 Mafunzo kwa Wajumbe kuhusu Muundo na Majukumu ya Wizara**

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoelezwa hapo awali, Wajumbe wa Kamati hii waliteuliwa kwa mara ya kwanza mwezi Januari, 2016. Hivyo, kwa kuzingatia jukumu la Kamati la kuzisimamia Wizara za Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mambo ya Ndani ya Nchi na ile ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wajumbe walipatiwa mafunzo haya ili waweze kufahamu kwa kina kuhusu Muundo na Majukumu ya Wizara hizo pamoja na Sera na Sheria mbalimbali zinazosimamiwa na Wizara hizo. Mafunzo haya yalifanyika mwezi Februari, 2016.



### 1.4.3 Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji za Wizara

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na Taasisi zake. Taarifa hizo ni kama zifuatazo:-

i) Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu:-

- Utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki mafanikio na changamoto kwa Kipindi cha Julai hadi Disemba, 2016;
- Utekelezaji wa majukumu ya Chuo cha Diplomasia, mafanikio na changamoto;
- Taarifa ya Sekretarieti ya *African Peer Review Mechanism* (APRM) Tanzania kuhusu utekelezaji wa majukumu yake, mafanikio na changamoto;
- Utekelezaji wa majukumu ya *Arusha International Conference Centre* (AICC), mafanikio na changamoto;
- Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi na nafasi ya Tanzania katika Uchumi wa dunia;
- Hatua iliyofikiwa katika kutatua mgogoro wa mpaka kati ya Tanzania na Malawi;
- Mikataba ya Kimataifa iliyosainiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ambayo haijaridhiwa na Bunge; na
- Utekelezaji wa Hati za Mkubaliano zilizosainiwa kati ya Tanzania na China wakati wa Ziara ya Rais wa Jamhuri ya Watu wa China iliyofanyika nchini Mwanzoni mwa Mwaka 2016;

ii) Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu:-

- Utekelezaji wa Sheria Namba 14 ya Mwaka 2007 ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, mafanikio na changamoto;
- Utekelezaji wa Majukumu ya Idara ya Wakimbizi mafanikio na changamoto wanazokabiliana nazo;
- Changamoto zinazoikabili Serikali baada ya kutoa Uraia kwa Wakimbizi katika kambi za wakimbizi Mishamo, Katumba na Ulyankulu; na
- Jeshi la Polisi kuhusu mikakati iliyopo ya kuzuia uhalifu nchini, mafanikio na changamoto.

iii) Taarifa ya Ofisi ya Rais- Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu hali ya Ulinzi na Usalama wa mipaka ya nchi na Usalama wa Raia na Mali zao;

iv) Taarifa ya Wizara ya Ulinzi na JKT kuhusu:-

- Utekelezaji wa majukumu ya Chuo cha Ulinzi wa Taifa, mafanikio na changamoto;na
- Hali halisi ya ulinzi katika maeneo ya Ziwa Nyasa kufuatia mgogoro wa mpaka kati ya Tanzania na Malawi.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa Wizara na Taasisi zake ilikuwa ni kutekeleza jukumu la kibunge la kuisimamia Serikali kama inavyotajwa katika Ibara ya 63 ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Baada ya kujadili taarifa hizo, Kamati ilibaini masuala mbalimbali ambayo yanafafanuliwa katika sehemu ya tatu ya taarifa hii.

#### **1.4.4 Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza matakwa ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kuhusu Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya

Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoishia, Kamati yangu ilikagua miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara inazosisimbia na iliyotengewa fedha kwa mwaka 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika**, miradi iliyokaguliwa na Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ipo chini ya vifungu vifuatavyo:-

- Fungu 34- Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;
- Fungu 29- Magereza;
- Fungu 93- Uhamiaji;
- Fungu 51- Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi;
- Fungu 38- Ngome; na
- Fungu 57- Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

Jumla ya miradi 13 ilikaguliwa na miradi hiyo imeambatanishwa katika taarifa hii (Tazama kiambatisho Na. 1)

**Mheshimiwa Spika**, katika ukaguzi huo, Kamati ilibaini masuala mbalimbali yalioathiri utekelezaji wa miradi hiyo. Masuala hayo yanaelezwa kwa kina katika sehemu ya tatu ya taarifa hii.

#### **1.4.5 Kuchambua Taarifa za Wizara kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016; na makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (2) ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane Kifungu cha 7(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Kamati yangu ilichambua taarifa za utekelezaji wa bajeti za Wizara inazosisimbia kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 kwa ajili ya kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

#### **1.4.6 Mapitio ya Taarifa za Wawakilishi wa Bunge katika SADC PF, PAP, IPU na EALA**

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoielezwa hapo awali, moja ya majukumu ya Kamati hii ni kushughulikia taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Vyama mbalimbali vya Kibunge na katika Bunge la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika. Jukumu hili limeainishwa katika Kifungu cha 7 (2) (iii & iv) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Kamati ilifanya mapitio ya taarifa za Wawakilishi wa Bunge katika SADC - PF, PAP, IPU na taarifa ya Wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki. Nakala za Taarifa za Wawakilishi hao zimeambatishwa na Taarifa hii. Nakala hizo ni:-

- i) Taarifa ya Wawakilishi wa Bunge la Dunia (IPU) (Kiambatisho Na. 2)
- ii) Taarifa ya Wawakilishi wa Bunge la Afrika (PAP) (Kiambatisho Na. 3)
- iii) Taarifa ya Wawakilishi wa Bunge katika Jumuiya ya Maendeleo ya Mabunge katika Nchi za kusini mwa Afrika (SADC- PF) (Kiambatisho Na. 4)
- iv) Taarifa ya Wabunge wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki (Kiambatisho Na. 5)

### **SEHEMU YA PILI**

#### **2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI**

##### **2.1 Maelezo ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuainisha majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia Januari 2016 hadi

Januari 2017, naomba sasa nitoe taarifa kuhusu masuala mbalimbali ambayo Kamati imeyabaini wakati ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, masuala yatakayotolewa taarifa ni yale ambayo Kamati imebaini kuwa changamoto zake zinahitaji kupewa umuhimu wa kipekee ili kuziwezesha Wizara pamoja na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kuleta tija kwa Taifa. Masuala hayo ni:-

**a) Masuala ya Ujumla**

- Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;

**b) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

- Msongamano wa wafungwa na mahabusu katika magereza;
- Uhalifu katika jamii;
- Ajali za Barabarani;
- Madeni ya muda mrefu ya Majeshi ya Polisi, Magereza na Idara ya Uhamiaji;
- Utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;
- Upungufu wa Sheria namba 14 ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ya Mwaka 2007;
- Wakimbizi wa Burundi waliopewa Uraia wa Tanzania;na
- Wahamiaji haramu.

**c) Wizara ya Ulinzi na JKT**

- Marekebisho ya Sheria Namba 16 ya Jeshi la Kujenga Taifa ya Mwaka 1964 (National Service Act 1964)
- Sera ya Taifa ya Ulinzi (The National Defence Policy);
- Alama za Mipaka ya Nchi; na
- Idadi ya vijana wanaotakiwa kujiunga na JKT kwa Mujibu wa Sheria.

#### **d) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

- Utendaji wa *African Peer Review Mechanism*;
- Utendaji wa Chuo cha Diplomasia;
- Utaratibu wa kuzipatia fedha Balozi za Tanzania zilizoko nje ya nchi
- Fedha kwa ajili ya safari za viongozi nje ya nchi kwenye Fungu la Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;
- Uchakavu wa Majengo ya Balozi za Tanzania nje ya Nchi;
- Utatuzi wa mgogoro wa Mpaka kati ya Tanzania na Malawi;
- Sera Mpya ya Mambo ya Nje (New Foreign Policy); na
- Mikataba na Itifaki iliyosainiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

#### **e) Uwakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Vyama mbalimbali vya Kibunge**

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwenye masuala yaliyoainishwa hapo juu katika sehemu ya taarifa inayofuata.

### **2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati**

#### **2.2.1 Upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) na kufanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 kwa Wizara zote inazosisimamia.

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara hizo, Kamati ilibaini kuwa baadhi ya miradi iliyotembelewa haikutekelezwa kutokana na kutopatiwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. Kwa mfano, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilitengewa jumla ya Shilingi **8,000,000,000.00** ambazo hadi Kamati inakagua miradi iliyoidhinishwa fedha nchini Msumbiji na Sweden Mwezi Juni, 2016, fedha hizo zilikuwa hazijatolewa.

Hata hivyo, Kamati imepokea taarifa kuwa hadi kufikia mwezi Disemba, 2016 Wizara ilikuwa imepokea Shilingi **3,489,315,000.00** sawa na asilimia 43.6 ya bajeti ya maendeleo. Kati ya fedha hizo Shilingi **1,316,435,000.00** ni kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa jengo la ghorofa tisa lililopo Ubalazi wa Tanzania Maputo, Msumbiji na Shilingi **2,172,880,000.00** kwa ajili ya ukarabati wa makazi ya Balazi na nyumba za watumishi zilizopo Stockholm, Sweden. Ni imani ya Kamati kuwa fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya miradi hiyo zitatolewa kwa ukamilifu wake hadi kufikia Mwezi Juni, 2017.

Vilevile, Wizara ya Ulinzi na JKT iliidhinishwa Jumla ya Shilingi **232,137,958,000.00** kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, hadi kufikia Mwezi Machi, 2016 Wizara ilipokea kiasi cha Shilingi **40,000,000,000.00**, sawa na asilimia 17.2 tu ya bajeti yote ya maendeleo. Hali kadhalika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi 5,984,023,924** kati ya **Shilingi 79,689,945,000.00** zilizoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 7.5 tu ya bajeti yote ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kubaini kuwa fedha za maendeleo zimekuwa hazitolewi kama zilivoidhinishwa na Bunge, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu mwenendo wa upatikanaji wa fedha za maendeleo katika kipindi cha miaka mitano kuanzia 2011/2012 hadi 2015/2016 kwa Wizara inazosisimamia.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa fedha za maendeleo zimeendelea kutolewa pungufu ikilinganishwa na Bajeti halisi inayopitishwa na Bunge, hali ambayo imeendelea kuathiri utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, kama inavyoonekana kwenye mfano unaotolewa hapa chini kwa Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (Fungu 57).

**MWENENDO WA FEDHA ZA MAENDELEO KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA, FUNGU 57 (2011/2012- 2015/2016)**

	<b>BAJETI ILIYOIDHINISHWA</b>	<b>FEDHA ZILIZOTOLEWA</b>	<b>FEDHA ZILIZOTOLEWA (%)</b>
2011/2012	129,017,767,000.00	129,000,000,000.00	99%
2012/2013	389,186,566,000.00	218,000,000,000.00	56%
2013/2014	229,582,027,000.00	87,216,816,585.00	37%
2014/2015	229,842,500,000.00	70,500,000,000.00	30%
2015/2016	220,137,958,000.00	40,000,000,000.00	18%

**Chanzo: Taarifa ya Wizara**

### **2.2.2 Msongamano wa wafungwa katika Magereza**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuendelea kuwepo kwa tatizo sugu la msongamano wa wafungwa na mahabusu katika Magereza nchini. Pamoja na mambo mengine, hali hii inachangiwa sana na:-

- i) Uwepo wa magereza machache nchini ikilinganishwa na idadi ya wafungwa/mahabusu;
- ii) Matumizi hafifu ya Sheria zinazoruhusu adhabu mbadala kwa wafungwa kama vile kifungo cha nje na mpango wa *Parole* wa huduma kwa jamii;
- iii) Kutotolewa maamuzi kwa wafungwa wa muda mrefu waliohukumiwa kunyongwa;
- iv) Wahamiaji haramu wanaokamatwa kwa makosa ya kuingia nchini isivyo halali kukaa magerezani kwa muda mrefu;
- v) Kutokupatikana kwa nakala za hukumu za kesi kwa ajili ya kukata rufaa;na
- vi) Kutosikilizwa kwa muda mrefu kwa kesi za mauaji na madawa ya kulevya.



### 2.2.3 Jeshi la Polisi linavyopambana na Uhalifu katika Jamii

**Mheshimiwa Spika**, Majukumu ya Jeshi la Polisi yameainishwa katika Kifungu cha 5 cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Watoa Huduma Wasaidizi wa polisi Sura ya 322 kama ilivyoboreshwa mwaka 2002. Majukumu hayo ni pamoja na kulinda amani, kulinda raia na mali zao, kuzuia makosa kabla hayajatendeka, kuwakamata wahalifu na kuwafikisha mahakamani na kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni za nchi.

**Mheshimiwa Spika**, uwezo wa Jeshi la Polisi wa kukabiliana na matukio mbalimbali ya uhalifu hauna budi kuwa na uwiano na idadi ya matukio ya uhalifu nchini. Hata hivyo, uwiano huo haupo kutokana na ongezeko kubwa la watu ukilinganisha na idadi ya askari, uchache wa vitendea kazi na uhaba wa fedha<sup>1</sup>.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokuwa ikichambua Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa Fungu 28- Jeshi la Polisi, ilibaini kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya Operesheni maalum za kuzuia uhalifu hazitoshelezi mahitaji halisi. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Jeshi hilo lilitengewa Tsh. 969,700,000/= tu kwa ajili ya shughuli hiyo. Hali hii inaathiri kwa kiasi kikubwa juhudi za utekelezaji wa mikakati ya Jeshi hilo katika kupunguza uhalifu katika Jamii.

### 2.2.4 Ajali za Barabarani

**Mheshimiwa Spika**, ajali za barabarani zimeendelea kusababisha athari nyingi za kiuchumi na kijamii kwa taifa na wahanga wa ajali. Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani, kwa mwaka 2016 ajali 9,856 zilirekodiwa na kusababisha vifo 3,256 na majeruhi 8,958 kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini.

---

<sup>1</sup> Takwimu ya Hali ya Uhalifu nchini Januari, 2015

**MCHANGANUO WA AJALI, VIFO NA MAJERUHI KWA AINA YA VYOMBO  
VILIVYOSABABISHA AJALI ZA BARABARANI KWA MWAKA 2016**

<b>AINA YA CHOMBO</b>	<b>AJALI</b>	<b>%</b>	<b>VIFO</b>	<b>%</b>	<b>MAJERUHI</b>	<b>%</b>
MAGARI BINAFSI	3,649	37.0	758	23.3	2,170	24.2
MABASI (PSV)	346	3.5	344	10.6	1,319	14.7
DALADALA (PSV)	947	9.6	342	10.5	1,379	15.4
TAXI CAB (PSV)	166	1.7	51	1.6	108	1.2
MAGARI YA KUKODI (PSV)	120	1.2	71	2.2	125	1.4
MAROLI YA TELA(HDV)	920	9.3	513	15.8	955	10.7
PIKIPIKI	2,544	25.8	890	27.3	2,128	23.8
BAISKELI	271	2.7	149	4.6	193	2.2
PICK-UPS	884	9.0	136	4.2	573	6.4
MIKOKOTENI	9	0.1	2	0.1	8	0.1
<b>JUMLA</b>	<b>9,856</b>	<b>100.0</b>	<b>3,256</b>	<b>100.0</b>	<b>8,958</b>	<b>100.0</b>

2

**Mheshimiwa Spika**, Takwimu zinaonesha kuwa vyanzo vingi vya ajali zinazotokea Tanzania husababishwa na makosa ya kibinadamu yanayohusisha matumizi mabaya ya watumiaji wa barabara. Kwa mujibu wa Taarifa za Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, makosa ya kibinadamu hasa yale yatokanayo na uzembe wa watumiaji wa barabara husababisha asilimia 76 ya ajali zote zinazotokea barabarani. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa asilimia 8 ya ajali zinachangiwa na ubovu wa miundombinu ya barabara na asilimia 16 ya ajali hizo husababishwa na ubovu wa vyombo vya moto vitumikavyo barabarani.

<sup>2</sup> Taarifa ya Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani 24/05/2016

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuainisha vyanzo hivyo vya ajali, Kamati imebaini kuwa Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973 ambayo ndio Sheria mama inayosimamia suala la usalama barabarani kwa kiasi kikubwa imeweza kukabiliana na tatizo la ajali barabarani. Hata hivyo, kutokana na utafiti uliofanywa na Asasi za kiraia zinazotetea mabadiliko ya Sheria na Sera ya Usalama barabarani, ilibainika kuwa Sheria ya Usalama barabarani ina mapungufu na haijitoshelezi kusaidia kupunguza tatizo sugu la ajali za barabarani<sup>3</sup>. Mapungufu ya Sheria yanaonekana katika visababishi vitano vya ajali ambavyo ni:-

- i) Mwendokasi;
- ii) Uvaaji wa kofia ngumu;
- iii) Ufungaji wa mikanda;
- iv) Matumizi ya kilevi; na
- v) Vizuizi vya watoto.

#### **2.2.5 Madeni ya muda mrefu ya Majeshi ya Polisi, Magereza na Idara ya Uhamiaji**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipopokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza na Idara ya Uhamiaji kwa kipindi cha Julai 2015 hadi Februari 2016, ilibaini kuwepo kwa tatizo la madeni ya muda mrefu. Madeni haya yanajumuisha madeni ya watumishi, wazabuni na malipo ya ankara za umeme, maji na simu. Kamati ilielezwa kuwa kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2009/2010 hadi 2014/2015 deni la Jeshi la Polisi lilikuwa limefikwa **Tsh. 385,033,500,342.50**; na kipindi cha kuanzia Mwaka 2012 hadi Desemba 2015, deni la Jeshi la magereza lilikuwa **Shilingi**

---

<sup>3</sup> Taarifa ya Muungano wa Asasi za Kiraia zinazotetea Mabadiliko ya Sheria na Sera ya Usalama Barabarani iliyowasilishwa kwenye Kamati tarehe 26/01/2017

**62,516,708,378.87**. Aidha, hadi kufikia mwezi Aprili 2016, Idara ya Uhamiaji lilikuwa linadaiwa Shilingi **5,627,974,474.00**

## **2.2.6 Utekelezaji wa Majukumu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ya Mwaka 2007**

**Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilianzishwa kwa Sheria Namba 14 ya Mwaka 2007. Sheria hii iliunganisha vikosi vyote vya zimamoto na uokoaji vilivyokuwa chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na vile vya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania Bara kuwa chini ya Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Aidha, Sheria hii inataja jukumu la msingi la Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni kukinga na kupunguza vifo, majeruhi na uharibifu wa mali unaotokana na moto, mafuriko, ajali za barabarani na dharura zote zisizo za jinai.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na nia njema ya Serikali ya kuanzisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa Sheria tajwa, Jeshi hilo limekuwa halipewi uzito unaostahili na kukabiliwa na changamoto mbalimbali zinazoathiri utendaji wake. Changamoto hizo ni pamoja na zifuatazo:-

- i) Uhaba wa vitendea kazi vikiwemo magari ya kuzimia moto, vifaa vya uokozi na visima vya kuhifadhia maji, hivyo kushindwa kuzima moto na kufanya uokozi kwa ufanisi zaidi;
- ii) Kushindwa kuyafikia maeneo mengi zaidi kwa ajili ya ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto kutokana na uchache wa rasilimali watu na magari ya ukaguzi;
- iii) Kushindwa kuzifikia wilaya zote nchini kwa lengo la kusogeza huduma za zimamoto na uokoaji karibu na wananchi kutokana na ukosefu wa rasilimali fedha. Aidha, ni Wilaya 15 tu kati ya Wilaya 141 nchini zenye vituo vya zimamoto na uokoaji; na
- iv) Kushindwa kuviunganisha vikosi vya Zimamoto na Uokoaji vilivyo chini ya Mamlaka ya Bandari na Viwanja vya Ndege kuwa chini ya

Kamandi ya Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kama Sheria inavyomtaka, hivyo kuleta ugumu katika kusimamia utekelezaji wa huduma za zimamoto na uokoaji nchini.

### **2.2.7 Upungufu wa Sheria Namba 14 ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (2007)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokutana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu utekelezaji wa Sheria Namba 14 ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mwezi Agosti, 2016, ilielezwa kuwa Sheria hii ina mapungufu mbalimbali na hivyo kuathiri utekelezaji wake. Baadhi ya Upungufu ulioelezwa ni pamoja na:-

- i) Sheria kutolipa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mamlaka ya kumiliki silaha jambo linalopelekea kushindwa kufanya majukumu yake ipasavyo hususan kwenye baadhi ya matukio ya uokoaji ambapo wananchi wanafanya fujo;
- ii) Sheria kutolipa Jeshi Mamlaka ya kukamata, jambo linalopelekea wananchi wengi kukaidi Sheria na Kanuni zake;
- iii) Sheria kutolitambua Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kama Mjumbe kwenye Tume ya Utumishi wa Polisi na Magereza, jambo linalosababisha ugumu katika kuwapandisha vyeo Maafisa wake; na
- iv) Sheria kutokutoa adhabu kali kwa wanaokaidi kufuata maelekezo ya Jeshi la Zimamoto hasa wale wanaogoma kulipa tozo na kutokufuata ushauri wa mifumo stahiki ya kufunga kwenye majengo yao.

### **2.2.8 Wakimbizi wa Burundi waliopewa uraia wa Tanzania kwa Mujibu wa Sheria**

**Mheshimiwa Spika**, Mnamo Mwaka 2014 Serikali ya Tanzania ilitoa uraia kwa wakimbizi wa Burundi 162,156 waliokuwa wakiishi katika makazi ya Mishamo, Katumba na Ulyankulu kwa zaidi ya miaka 40. Hata hivyo, pamoja na kuwa jambo hilo lilifanyika kwa nia njema, wakimbizi hao waliopewa uraia hawakusambazwa katika maeneo mbalimbali nchini na

badala yake waliachwa katika makazi yao ya awali kinyume na matakwa ya Sheria Namba 9 ya Wakimbizi ya Mwaka 1998, inayotaka wakimbizi pekee kuishi katika eneo la Makazi ya wakimbizi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipofanya ziara katika makazi ya Ulyankulu Mwezi Januari, 2017, ilibaini kutokuwepo kwa mpango wowote wa Serikali wa kuwahamisha wakimbizi wote waliopewa uraia kutoka katika makazi hayo, na hakukuwa na maandalizi yoyote ya maeneo watakayopelekwa raia hao wapya. Aidha, suala zima la wakimbizi bado lipo kwenye mchakato wa uboreshaji wake.

### **2.2.9 Sheria namba 16 ya Jeshi la Kujenga Taifa ya Mwaka 1964 (National Service Act 1964)**

**Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Kujenga Taifa lilianzishwa kwa Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa namba 16 ya Mwaka 1964. Sheria hii inatoa uwezo wa Jeshi la Kujenga Taifa kuandikisha vijana wa kulitumikia Jeshi hilo.

**Mheshimiwa Spika**, tangu kuanzishwa kwa JKT, Sheria hii imeshafanyiwa marekebisho yafuatayo:-

- Marekebisho ya Mwaka 1966 ambapo Sheria ilirekebishwa ili Jeshi liweze kuandikisha vijana wenye taaluma zaidi ya kidato cha nne kwa mujibu wa Sheria; na
- Marekebisho ya Mwaka 1975 ambapo Sheria ilirekebishwa ili kuruhusu JKT kuungana rasmi na JWTZ kwa lengo la kuimarisha ulinzi wa Taifa na hivyo kulifanya JKT kuwa moja ya Kamandi zilizo chini ya JWTZ.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na marekebisho yaliyofanyika, Kamati imebaini kuwa kuna baadhi ya maeneo hayajatajwa kabisa katika Sheria hii na hivyo kuwepo na uhitaji wa kufanya marekebisho zaidi. Kwa mfano, suala la fidia kwa vijana wanaopata mafunzo ya JKT

halijatajwa chini ya Sheria hii ili kuwawezesha vijana walio kwenye mafunzo kupata fidia pale wanapoumia wakiwa mafunzoni.

### 2.2.10 Sera ya Taifa ya Ulinzi (The National Defence Policy)

**Mheshimiwa Spika**, Mchakato wa kuhuisha Sera ya Taifa ya Ulinzi ulianza tangu Bunge la 10 ambapo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama iliishauri Serikali katika Taarifa ya utekelezaji wa shughuli zake kwa Mwaka 2013, kuharakisha utayarishwaji wa Sera hii, na naomba kunukuu kipengele hicho kama ifuatavyo:-

‘Kuhusu utayarishwaji wa Sera na Sheria ya Ulinzi wa Taifa, Kamati inaishauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuwasiliana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar waweze kutoa maoni yao mapema iwezekanavyo yatakayoweza kukamilishwa kwa Sera ya Taifa ya Ulinzi na hatimaye Sheria ya Taifa ya Ulinzi na Usalama’<sup>4</sup>

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa hadi sasa Sera hii haipo na Serikali inaendelea kutoa maelezo kuwa mchakato unaendelea.

### 2.2.11 Alama za Mipaka ya Nchi

**Mheshimiwa Spika**, wakati ikitekeleza majukumu yake, Kamati ilibaini kuendelea kuwepo kwa tatizo la kukosekana/kung’olewa kwa alama za mipaka (beacons) katika maeneo mengi ya mipaka ya nchi. Pamoja na kwamba Kamati hii imekuwa ikizungumzia kuwepo kwa tatizo hili, bado hakuna hatua za kuridhisha zilizochukuliwa na Serikali ili kulimaliza.

### 2.2.12 Idadi ya vijana wanaotakiwa kujiunga na JKT kwa mujibu wa Sheria

**Mheshimiwa Spika**, vijana wanaojiunga na JKT kwa mujibu wa Sheria ni wale wanaohitimu Kidato cha Sita, na kila mwaka takribani vijana 60,000 wanamaliza Kidato cha Sita. **Hata hivyo**, Jeshi la Kujenga Taifa lina uwezo wa kuchukua vijana wa kujiunga na JKT kwa Mujibu wa Sheria wapatao 35,000 tu.

---

<sup>4</sup> Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama 2013:16

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uwezo wa JKT kutoa mafunzo kwa vijana wachache ikilinganishwa na idadi ya wahitimu, Kamati imebaini kuwa JKT inashindwa kutoa mafunzo kwa vijana 35,000 ambao ndio uwezo wa Jeshi hilo. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 ni vijana 20,100 tu walipatiwa mafunzo na kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 idadi hiyo ilipungua kufikia 14,000. Kamati ilielezwa kuwa upungufu huu unasababishwa na ukosefu wa fedha ambapo kati ya Shilingi Biloni 8 zilizotengwa kwa ajili hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, ni Shilingi Biloni 1 tu iliyotolewa sawa na asilimia 12.5.

### **2.2.13 Utendaji wa *African Peer Review Mechanism (APRM)* - Tanzania**

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote, Kamati inampongeza Balozi Ombeni Sefue kuingizwa kwenye Kamati ya watu mashuhuri wa Afrika katika Mpango huu.

**Mheshimiwa Spika**, APRM ni Mpango wa Nchi 35 za Kiafrika wa Kujitathmini kwa vigezo vya Utawala Bora. Mpango huu unalenga kukuza maendeleo ya nchi za kiafrika, Tanzania ikiwa mojawapo, kwa kuimarisha utawala bora katika nchi hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokutana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mwezi Agosti, 2016, ilielezwa kuwa pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kutekeleza majukumu ya APRM-Tanzania, bado kuna changamoto mbalimbali zinazoathiri utendaji wake. Changamoto hizo ni:-

- i) Upungufu wa fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kwa mfano, kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 mahitaji halisi yalikuwa **Shilingi 1,765,000,000.00**, wakati fedha zilizoidhinishwa na Bunge zilikuwa **Shilingi 620,160,000.00** sawa na asilimia 35 tu ya mahitaji halisi. Fedha hizi zilitumika kulipa Mishahara na kugharamia mambo madogo madogo ya uendeshaji na hakukuwa na fedha



yoyote kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizokusudiwa kama vile kushindwa kutoa taarifa kwa wananchi kuhusu matokeo ya tathmini ya utawala bora katika nchi yao;

- ii) APRM - Tanzania kutokuwa na hadhi ya Kisheria (Legal Entity). Hii inaikwamisha Taasisi hii kuwa Idara inayojitegemea chini ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, kukosekana kwa hadhi ya kisheria kunazuia APRM - Tanzania kuwa na Kasma yake na kutengewa bajeti kulingana na mahitaji yake;
- iii) Malimbikizo ya michango ya uanachama wa Tanzania katika APRM Afrika ambapo mpaka Mwezi Agosti 2016, Tanzania ilikuwa haijachangia kiasi cha Dola za Kimarekani 396,032 sawa na Shilingi 871,240,000.000 ikiwa ni deni la Miaka Mitatu; na
- iv) Uchakavu wa vitendea kazi kama vile magari na vifaa vya ofisini ambapo kwa mara ya mwisho magari na vifaa vilivyopo vilinunuliwa Mwaka 2007 wakati Sekretarieti ya APRM Tanzania inaanzishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijiridhisha kuwa changamoto tajwa hapo juu ndizo zinazoathiri utendaji wa Taasisi ya APRM - Tanzania.

#### **2.2.14 Utendaji wa Chuo cha Diplomasia**

**Mheshimiwa Spika**, jukumu kubwa la Chuo cha Diplomasia ni kutoa mafunzo na kufanya utafiti katika masuala ya Diplomasia, uhusiano wa Kimataifa, Stratejia na usuluhishi wa migogoro na ujenzi wa amani. Hata hivyo, Chuo hiki kimeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali zinazoathiri utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, ni vyema kutambua kuwa, Chuo hiki kilianzishwa Mwaka 1978 kwa ushirikiano wa Serikali mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Msumbiji. Kwa Miaka Mitano tangu Chuo

kilipoanzishwa nchi zote mbili zilishiriki katika uendeshaji wake. Hata hivyo, tangu Mwaka 1982 hadi sasa, Msumbiji iliacha kuchangia katika bajeti na kushiriki katika shughuli za uendeshaji, hivyo gharama zote za uendeshaji wa chuo zikabaki kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Msumbiji kujitoa katika ushiriki wa uendeshaji wa chuo hiki ni mojawapo ya changamoto zinazokikabili chuo. Changamoto nyingine ni pamoja na:-

- i) Gharama kubwa za uendeshaji wa Chuo na ufinyu wa bajeti ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 Chuo kilitengewa bajeti ya matumizi mengineyo ya **Shilingi 2,524,570,000.00** na hadi kufikia Mwezi Juni 2015 kiasi kilichotolewa kilikuwa **Shilingi 767,553,532.00** sawa na asilimia 30 tu ya fedha zilizoidhinishwa. Aidha, ufinyu wa bajeti unasababisha malimbikizo ya madeni ambapo hadi kufikia Mwezi Juni 2016 Chuo kilikuwa kinadaiwa la **Shilingi 1,809,347,196.00**; na
- ii) Ukosefu wa miundombinu ya kutosha hasa majengo ambapo yale yanayotumika hivi sasa mengi ni ya zamani na hayakidhi ongezeko la udahili na idadi ya wafanyakazi.

#### **2.2.15 Balozi za Tanzania nje ya Nchi kutopata fedha kwa wakati**

**Mheshimiwa Spika**, kwa muda mrefu Balozi zetu zimekuwa zikikabiliwa na changamoto ya kutopata fedha kwa wakati. Jambo hili limeendelea kuathiri ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Balozi hizo, licha ya ushauri unaotolewa na Kamati hii kuanzia Bunge la Kumi kuhusu utaratibu wa Hazina kupeleka fedha moja kwa moja kwenye Balozi hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kuwa Serikali bado haina nia thabiti ya kutekeleza ushauri huo kwani upatikanaji wa fedha katika Balozi nyingi haupo katika mtiririko wa kuridhisha.

## **2.2.16 Fedha za safari za Viongozi nje ya nchi kwenye Fungu la Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutenga fedha za safari za Viongozi nje ya nchi kwenye Fungu la Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Tangu Mwaka wa Fedha 2010/2011 Kamati ilishauri malipo ya safari za Viongozi nje ya nchi yagharimiwe moja kwa moja kwa mafungu yaliyo chini ya Hazina, hata hivyo ushauri huu haujatekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, hali hii inapelekea Fungu la Wizara kuonekana limetengewa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake ilihali katika hali halisi fedha nyingi huwa ni kwa ajili ya safari za Viongozi na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yake ya msingi.

## **2.2.17 Uchakavu wa majengo ya Balozi za Tanzania**

**Mheshimiwa Spika**, majengo ya baadhi ya Balozi zetu yameendelea kuwa chakavu kutokana na kutofanyiwa ukarabati kwa muda mrefu. Kamati yangu ilipofanya ziara ya ukaguzi wa mradi wa ukarabati wa majengo katika Ubalozi wa Tanzania nchini Sweden Mwezi Juni, 2016, ilishuhudia uchakavu uliokithiri wa majengo ya makazi ya Balozi na Nyumba za Watumishi wa Ubalozi huo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa majengo yote mawili yalitakiwa kufanyiwa ukarabati tangu Mwaka wa Fedha 2014/2015 lakini kutokana na uhaba wa fedha ukarabati huo haukufanyika na hivyo kusababisha kutotumika kwa sasa. Ni dhahiri kuwa hali hii inaathiri taswira ya nchi yetu nje ya nchi.

## **2.2.18 Utatuzi wa Mgogoro wa mpaka kati ya Tanzania na Malawi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu hatua zilizofikiwa katika kutatua mgogoro wa mpaka kati ya Tanzani na Malawi na hivyo

ilikutana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mwezi Oktoba, 2016.

Katika kikao hicho, Kamati ilielezwa kuwa mgogoro wa mpaka kati ya nchi hizi mbili unatokana na kutokukubaliana kuhusu mapitio ya mpaka kwenye Ziwa Nyasa. Aidha, ilielezwa kuwa kiini cha mgogoro huo ni Mkataba wa Heligoland uliowekwa saina kati ya Uingereza na Ujerumani tarehe 01 Julai, 1890, ambapo Ibara ya 1(2) ya Mkataba huo inaeleza kuwa:-

“...to the south by a line which, starting on the coast at the northern limit of the province of Mozambique, follows the course of the river Ruvuma to the point of confluence of the Msinje; thence it runs westwards along the parallel of the t point till it reaches Lake Nyassa; thence striking northwards it follows the eastern, northern and western shores of the lake to the northern bank of the mouth of River Songwe; it ascends that river....”

**Mheshimiwa Spika**, Ibara hiyo ndio iliyosimamiwa na nchi ya Malawi kuwa inawapa umiliki wa Ziwa lote. Hata hivyo, Tanzania yenyewe imesimamia Ibara ya VI inayoeleza kuwa:-

“All the lines of demarcation traced in articles 1 to IV shall be subject to rectification by agreement between the two powers in accordance with local requirements”

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Tanzania ina msimamo kuwa ibara inayosimamiwa na Malawi haina maana yoyote hadi hapo mpaka huo utakapopimwa kwa kuzingatia uhalisia wa mazingira na kuridhiwa na pande zote mbili, ambapo kwa mujibu wa ibara ya VI ya Mkataba huo Kamisheni ya Mipaka ilifanya marekebisho na kuuhamisha mpaka huo katikati ya mto Songwe kupitia Mkataba wa Mwaka 1901.

**Mheshimiwa Spika**, mpaka sasa nchi zote mbili zimeshikilia misimamo yake japokuwa zipo tayari kwa usuluhishi wa mgogoro huo. Pande zote mbili ziliafiki kuwasilisha ombi la kusuluhishiwa mgogoro huo kwenye jopo la Viongozi Wastaafu wa Afrika wa nchi za SADC kutoka Msumbiji, Afrika Kusini na Botswana Mwezi Disemba 2012. Usuluhishi huo unaendelea chini ya Uenyekiti wa Mhe. Joachim Chissano, Rais Mstaafu wa Msumbiji akisaidiwa na Mhe. Festus. Mogae, Rais Mstaafu wa Botswana na Mhe. Thabo Mbeki, Rais Mstaafu wa Afrika Kusini.

**Mheshimiwa Spika**, Jitihada za usuluhishi kwa njia ya kidiplomasia bado zinaendelea ambapo majadiliano ya mwisho yamefanyika tarehe 24 Januari, 2017 ambayo yanatarajiwa kuendelea mwezi wa Aprili, 2017. Ni matumaini ya Kamati yangu kuwa mgogoro huo utamalizika kwa njia za amani na salama.

### **2.2.19 Sera Mpya ya Mambo ya Nje**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeendelea kusimamia utekekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje. Sera hii, pamoja na mambo mengine, ina lenga kukuza na kuendeleza Diplomasia ya uchumi nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokutana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mwezi Machi, 2016, ilielezwa kuwa Sera hii Mpya ya Mambo ya Nje ilitungwa Mwaka 2001. Ni dhahiri kuwa Sera hii imeendelea kutumika kwa muda mrefu bila kuzingatia mabadiliko ya sasa ya Kiuchumi, Kisiasa, Kijamii na mazingira yanayotokea duniani.

### **2.2.20 Mikataba iliyosainiwa kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Nchi Nyingine**

**Mheshimiwa Spika**, moja ya majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni kuratibu na kusimamia Mikataba na makubaliano ya kimataifa. Lengo la Mikataba hii ni kuiwezesha nchi yetu

kuimarisha na kudumisha ushirikiano wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Kimataifa na Kikanda kwa maslahi ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na lengo zuri la Mikataba inayosainiwa kati ya nchi yetu na nchi nyingine, Kamati imebaini kuwepo kwa mikataba mingi iliyosainiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini haijaridhiwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokutana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mwezi Januari, 2017 ilielezwa kuwa Mikataba isiyopungua 43 ambayo imesainiwa, bado haijaridhiwa na Bunge. Taarifa hiyo ilionesha Mikataba iliyosainiwa ni ile ya kuanzia Mwaka 1972 hadi 2016.

Kamati ilielezwa kuwa, Mikataba mingi iliyokwisha kusainiwa huchelewa kuletwa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa kwa kuwa inapaswa kufanyiwa tathmini ya kina ili kujua umuhimu na manufaa yake kwa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na nia njema ya kujiridhisha kuhusu manufaa ya Mikataba hiyo kwa Taifa letu, ni dhahiri kuwa baadhi ya Mikataba ni ya muda mrefu na Kamati haiafiki kuwa Serikali inahitaji zaidi ya Miaka Mitano au Kumi kujiridhisha kuhusu manufaa ya Mikataba hiyo.

#### **2.2.21 Wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano katika Vyama mbalimbali vya Kibunge**

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoelezwa hapo awali, Bunge letu huwakilishwa kwenye Vyama mbalimbali vya Kibunge vikiwemo CPA, ACP- EU na IPU, na kwenye Mabunge ya SADC (SADC- PF), Bunge la Afrika (PAP) na Bunge la Afrika Mashariki (EALA). Uwakilishi huu, pamoja na mambo mengine, ni njia mojawapo ya kutekeleza Diplomasia ya Kibunge ambapo, wawakilishi hawa wakishiriki ipasavyo mikutano ya Vyama hivyo vya Kibunge na Mabunge hayo, huliongezea Bunge lako Tukufu uwezo wa ushawishi wa kibunge katika Afrika, Kanda ya SADC,

Afrika Mashariki na Jumuiya ya Madola. Aidha, uwakilishi huu unalipa Bunge lako nguvu ya kuchochea kasi ya kuridhia Mikataba ya Kimataifa iliyosainiwa na Tanzania pale ambapo Mikataba hiyo inaonekana kuwa na tija Kiuchumi, Kisiasa na Kijamii kwa Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na umuhimu mkubwa wa wawakilishi hawa katika kutekeleza Diplomasia ya Kibunge, Kamati imebaini kuwa katika kipindi cha Januari 2016 - Januari 2017, baadhi ya Wawakilishi wameshindwa kuhudhuria mikutano ya Mabunge/ Vyama vya Kibunge, na wengine kuchelewa kuwasili katika vikao hivyo kutokana na kuchelewa kupatikana kwa vibali vya kusafiri nje ya nchi. Hali hiyo iliathiri fursa ya kushiriki ipasavyo katika masuala muhimu yaliyokuwa yanajadiliwa katika mikutano hiyo.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

#### 3.1 Maoni

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuwasilisha matokeo ya uchambuzi wa Kamati katika Sehemu ya Pili, naomba sasa kuwasilisha maoni ya Kamati katika maeneo hayo kama ifuatavyo:-

##### a) Masuala ya Jumla

- i) Kutokutolewa kwa fedha za maendeleo kunaathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye Wizara zote tatu tunazosisimamia.

##### b) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

- ii) Kutotekelezwa kwa Sheria ya Msamaha (Parole) na Sheria ya *Community Service* nchini kunachangia kwa kiasi kikubwa msongamano wa wafungwa magerezani;

- iii) Kutokusikilizwa kwa kesi kwa haraka kunasababisha msongamano wa mahabusu magerezani hususan kesi za mauaji, madawa ya kulevya, n.k;
- iv) Kutotolewa maamuzi kwa wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kunyongwa kunachangia msongamano wa wafungwa wa aina hiyo;
- v) Kutokuwarudisha makwao wahamiaji haramu wanaokamatwa kwa makosa ya kuingia nchini isivyo halali kunaiongezea Serikali gharama za kuwatunza wahamiaji hao magerezani;
- vi) Kutokupatikana kwa nakala za hukumu za kesi kwa ajili ya kukata rufaa kunachangia malalamiko mengi ya wafungwa kutotendewa haki yao kikatiba;
- vii) Msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani pamoja na kuhatarisha afya za wafungwa, unaiongezea Serikali gharama za kuwatunza wafungwa na mahabusu;
- viii) Kutosambazwa kwa wakimbizi wa Burundi waliopewa uraia wa Tanzania katika maeneo mbalimbali nchini kuna hatarisha hali ya ulinzi na usalama katika maeneo ya makazi; Aidha, kutosambazwa kwa raia hao wapya ni kinyume cha matakwa ya Sheria Namba 9 ya Wakimbizi ya Mwaka 1998;
- ix) Kutokupewa fedha za kutosha Jeshi la Polisi ili wakabiliane na uhalifu mbalimbali nchini kutawafanya Polisi wasikabiliane na wahalifu hao kwa ukamilifu;
- x) Kutotenga fedha za kutosha kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kunaathiri utekelezaji wa majukumu ya Msingi ya Jeshi hilo;
- xi) Upungufu uliopo kwenye Sheria namba 14 ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji unapunguza ufanisi katika utekelezaji wa Sheria hiyo;



- xii) Kutokuwepo kwa mfumo wa mawasiliano ya kielektroniki ambao unaziunganisha Ofisi za Uhamiaji Mkoa, Wilaya, Vituo vya Mipakani na makao makuu kunaathiri udhibiti wa uingiaji na utokaji wa watu hususan utambuzi wa wahamiaji haramu;

**c) Wizara ya Ulinzi na JKT**

- xiii) Kutokutolewa mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana wote wanaohitimu Kidato cha Sita kunachangia kupunguza uzalendo na kuzorotesha maadili ya vijana wengi nchini;
- xiv) Kukosekana kwa Sera ya Ulinzi wa Taifa nchini (National Defence Policy) kunaathiri ufanisi katika uratibu wa ulinzi wa Taifa.

**d) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

- xv) Utaratibu wa kutuma fedha kwenye Balozi zetu nje ya nchi kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki unaathiri utekelezaji wa majukumu ya msingi katika Balozi hizo;
- xvi) Kukosekana kwa Balozi ndogo/uwakilishi wa heshima kwenye baadhi ya miji yenye fursa nyingi za kiuchumi kunaathiri malengo ya Serikali ya kukuza uchumi wa nchi kupitia Diplomasia ya uchumi;
- xvii) APRM Tanzania kutokuwa na hadhi ya Kisheria (legal entity) kunaikwamisha Taasisi hii kuwa na Kasma yake ya Kibajeti na hivyo kuathiri utendaji wake kutokana na ufinyu wa bajeti;
- xviii) Malimbikizo ya michango ya uanachama wa Tanzania katika Taasisi ya APRM Afrika yanapunguza hadhi ya nchi yetu mbele ya jamii ya Kimataifa;
- xix) Kutokutolewa kwa elimu ya kutosha kwa Umma kuhusu APRM kunasababisha wananchi wengi wasijue kuhusu APRM na faida zake kwa nchi;

- xx) Ufinyu wa Bajeti ya matumizi ya kawaida na maendeleo kunachangia Chuo cha Diplomasia kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo hali inayoweza kusababisha Chuo hicho kufutiwa usajili na NACTE;
- xxi) Kutenga fedha kwa ajili ya safari za Viongozi nje ya nchi kwenye Fungu la Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kunaathiri utengwaji wa Bajeti yenye uhalisia wa Wizara hiyo kuweza kutekeleza majukumu yake;
- xxii) Kutokarabati majengo ya Balozzi zetu si tu kunashusha thamani ya majengo hayo yaliyonunuliwa kwa fedha nyingi, lakini pia yanaweza kushusha hadhi ya nchi yetu inayopewa heshima kubwa duniani;
- xxiii) Wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano katika vyama mbalimbali vya Kibunge kutoshiriki mikutano ya vyama hivyo kikamilifu kunaleta picha isiyo nzuri mbele ya Mabunge mengine ya Afrika na Duniani kwa ujumla kuwa Bunge lako Tukufu halithamini umuhimu wa Diplomasia ya Kibunge;
- xxiv) Kukosekana kwa kitengo maalum cha kufuatilia utekelezaji wa mikataba iliyosainia na Tanzania kunachewelesha mikataba mingi kufikishwa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa; na
- xxv) Sera ya Mambo Nje ni ya muda mrefu na haiendani na mabadiliko ya sasa ya Kiuchumi, Kiasia, Kijamii na mazingira yanayotokea duniani.

### **3.2 Mapendekezo**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza maoni ya Kamati, naomba kutoa mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

### 3.2.1 Kutokutolewa kwa fedha za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Kwa kuwa** utekelezaji wa miradi ya maendeleo hutegemea upatikanaji wa fedha na kwamba fedha kwa ajili ya miradi hiyo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 hazikupokolewa kutoka Hazina, jambo ambalo lilikwamisha utekelezaji wa miradi hiyo,

**Na kwa kuwa** kutokutekelezwa kwa miradi hiyo kutokana na kutopelekewa fedha kumesababisha hasara kwa kuwalipa wasimamizi wa miradi hiyo bila kutekeleza majukumu yao ya msingi,

**Kwa hiyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuteleza miradi ya maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge ili kufanikisha azma ya Serikali kwa miradi hiyo.

### 3.2.2 Msongamano wa Wafungwa na Mahabusu Magerezani

**Kwa kuwa** imebainika kuwa tatizo la msongamano wa wafungwa na mahabusu katika magereza nchini limeendelea kuongezeka kutokana na:

- i) Kutokutekelezwa ipasavyo kwa utaratibu wa *Parole*;
- ii) Kutokutumika kwa Sheria zinazohusu adhabu mbadala kwa wafungwa;
- iii) Kutokukutana ipasavyo kwa Kamati za Kusukuma kesi; na
- iv) Kutowezekana kutekelezwa kwa hukumu ya adhabu ya kunyongwa hadi kufa;

**Na kwa kuwa** hali hiyo inaathiri afya za wafungwa na mahabusu (watu ambao hawajahukumiwa) na kuingozea Serikali gharama za kuwatunza;

**Kwa hiyo basi,** Serikali:-

- i) Itekeleze ipasavyo utaratibu wa *Parole* kwa mujibu wa Sheria;
- ii) Itekeleza Sheria inayowataka wahalifu wenye makosa madogo kupewa adhabu ya vifungo vya nje ili watumikie jamii (*Community Service Act*);

- iii) Ihakikishe kuwa Kamati za kusukuma kesi zinakutana mara kwa mara ili kuwezesha hukumu za kesi hizo kutolewa kwa wakati; na
- iv) Itolee maamuzi suala la wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kunyongwa hadi kufa (condemned).

### 3.2.3 Kuwarejesha wahamiaji haramu

**Kwa kuwa** magereza mengi nchini yanakabiliwa na msongamano mkubwa wa wafungwa na mahabusu,

**Na kwa kuwa** kati ya wafungwa/mahabusu hao wengine ni wahamiaji haramu ambao hukaa kwa muda mrefu bila ya kurudishwa makwao,

**Kwa hiyo basi**, Serikali iwarudishe makwao wahamiaji hao ili kupunguza mzigo wa kuendelea kuwatunza katika Magereza yetu.

### 3.2.4 Makazi ya Wakimbizi ya Ulyankulu

**Kwa kuwa** makazi ya wakimbizi ya Ulyankulu yanakaliwa na watu 93,062 ambao kati yao 15,220 ni wazawa na 3,985 ni wakimbizi ambao hawana uraia wa Tanzania,

**Na kwa kuwa** Sheria Namba 9 ya Wakimbizi ya Mwaka 1998 inatamka kuwa mtu yeyote ambaye ni Raia haruhusiwi kukaa ndani ya makazi ya wakimbizi isipokuwa wakimbizi tu,

**Na kwa kuwa** eneo la makazi ya Ulyankulu lenye ukubwa wa Kilomita za mraba 1200 ilikuwa ni sehemu ya hifadhi ya Pori la Akiba la Ulyankulu, na watu wanaoishi katika eneo hilo wanaendelea na shughuli za kibinadamu kama vile kilimo na ufugaji ambazo zinaathiri uhifadhi wa mazingira katika eneo hilo,

**Kwa hiyo basi**, Serikali iweke utaratibu wa kutekeleza matakwa ya Sheria Namba 9 ya Wakimbizi ya Mwaka 1998 ili kuilinda hifadhi ya Pori la Akiba la Ulyankulu ambalo ni muhimu kwa ustawi wa mazingira katika ukanda ule. Aidha, pale itakapobidi, Serikali ifanye marekebisho ya Sheria Namba 9 ya Wakimbizi ili iendane na mazingira ya sasa ya wakimbizi.

### 3.2.5 Jeshi la Polisi Kukabiliana na Uhalifu

**Kwa kuwa** vitendo vya uhalifu mbalimbali katika jamii vimeendelea kuongezeka kwa kasi kubwa,

**Na kwa** kuwa Bajeti inayotengwa kwa ajili ya kuliwezesha Jeshi la Polisi kukabiliana na vitendo vya uhalifu ni ndogo ukilinganisha na mahitaji halisi ya mafuta, magari na vitendea kazi,

**Kwa hiyo basi** Serikali iongeze Bajeti ya Jeshi la Polisi ili liweze kukabiliana na uhalifu unaoendelea kufanyika. Aidha, kama ilivyo kwa mradi wa BRN wa Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni unaolenga kupunguza uhalifu kwa kiasi kikubwa katika Mkoa huo, Serikali ihamasishe uanzishwaji wa miradi ya aina hiyo katika Mikoa yote Tanzania.

### 3.2.6 Ajali za Barabarani

**Kwa kuwa** ajali za barabarani zimeendelea kusababisha athari nyingi kiuchumi na kijamii kwa Taifa,

**Na kwa kuwa** imebainika kuwa Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973 ina mapungufu na ikibaki kama ilivyo sasa itashindwa kupunguza tatizo hilo sugu linaloendelea kukua kila siku,

**Kwa hiyo basi**, Sheria hiyo ifanyiwe marekebisho kwa kuvielezea kwa kiwango kamili visababishi vyote vya ajali za barabarani ili kuweza kudhibiti na kupunguza ajali za barabarani.

### 3.2.7 Utaratibu wa kutuma fedha kwenye Balozi zetu nje ya nchi

**Kwa kuwa** utaratibu wa kutuma fedha kwenye Balozi zetu unataka fedha hizo zipitishwe katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki,

**Na kwa kuwa** utaratibu huo umebainika kuwa na urasimu usio wa lazima na hivyo kuchelewesha kutuma fedha kwa mtiririko unaotakiwa,

**Kwa hiyo basi**, Serikali ipeleke fedha za Balozi moja kwa moja bila kupitisha Wizarani kama ilivyo kwa Halmashauri zote nchini ambapo

fedha hutumwa moja kwa moja bia kupitisha kwa Makatibu Tawala wa Mikoa husika.

### 3.2.8 Uchakavu wa majengo ya Balozi za Tanzania

**Kwa kuwa** majengo mengi ya Balozi zetu nje ya nchi ni chakavu sana, **Na kwa kuwa** kutokarabati majengo hayo kumeendelea kuiongezea gharama Serikali kwani baadhi ya Balozi zinalazimika kukodi majengo mengine mbadala,

**Kwa hiyo basi**, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Serikali itenge fedha za ukarabati wa majengo ya Balozi kwa awamu kwa kuanza na Balozi ambazo majengo yake yapo katika hali mbaya zaidi kama vile majengo ya Ubalozi wa Tanzania nchini Sweden.

### 3.2.9 Uendelezaji wa viwanja vya Balozi za Tanzania

**Kwa kuwa** kumekuwa na changamoto ya kuendeleza viwanja vya Balozi zetu nje ya nchi kwa mfano kiwanja cha Ubalozi wa Tanzania mjini Maputo kilichopatikana Mwaka 1978,

**Na kwa kuwa** kutoviendeleza viwanja hivyo kunaisababishia Serikali kupoteza mapato na vilevile kuwepo uwezekano wa viwanja hivyo kuchukuliwa na Mamlaka za nchi husika,

**Kwa hiyo basi**, Serikali itafute fedha kutoka kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na vyanzo vingine kwa ajili ya kuviendeleza viwanja hivyo ambapo majengo yatakayojengwa yanaweza kutumika kama kitega uchumi na hivyo kuongeza pato la Serikali.

### 3.2.10 Sera Mpya ya Mambo ya Nje

**Kwa kuwa** Sera ya Mambo ya Nje (2001) imeendelea kutumika kwa muda mrefu,

**Na kwa kuwa** Sera hiyo kwa sasa haizingatii mabadiliko ya sasa ya Kiuchumi, Kisiaa, Kijamii na Kimazingira yanayotokea duniani,

**Hivyo basi**, Serikali iongeze kasi ya kufanya mapitio ya Sera ya Mambo ya Nje ili kuwa na Sera itakayozingatia kukuza na kuendeleza dhana ya Diplomasia ya Uchumi kwa mapana yake.

### **3.2.11 Utekelezaji wa Mikataba iliyosainiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**Kwa kuwa** ipo mikataba mingi na ya muda mrefu iliyosainiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini haijaridhiwa na Bunge,

**Na kwa kuwa** kutoridhiwa kwa Mikataba hiyo na Bunge lako tukufu kunachelewesha kuanza kwa utekelezaji wa mikataba hiyo,

**Hivyo basi**, Serikali ianzishe kitengo au Idara maalum ya kufuatilia utekelezaji wa mikataba iliyosainiwa na nchi yetu ili kuongeza ufanisi, tija na heshima ya nchi yetu.

### **3.2.12 Upatikanaji wa vibali vya kusafiri nje ya nchi kwa Wawakilishi wa Bunge katika Vyama Mbalimbali vya Kibunge**

**Kwa kuwa** baadhi ya Wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hawakuweza kushiriki kikamilifu mikutano ya vyama mbalimbali kutokana na kuchelewa kupata vibali vya kusafiri nje ya nchi,

**Na kwa kuwa** kutoshiriki vikao hivyo kunaleta picha isiyo nzuri mbele ya Mabunge mengine ya Afrika na Duniani kwa ujumla kuwa Bunge lako Tukufu halithamini umuhimu wa Diplomasia ya Kibunge,

**Hivyo basi**, Kamati inashauri Ofisi ya Bunge kuwa na utaratibu wa kuwasilisha Serikalini maombi ya vibali vya kusafiri nje ya nchi mapema kulingana na ratiba ya vikao hivyo, na vilevile Serikali itoe fedha na vibali hivyo kwa wakati muafaka.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 HITIMISHO

#### 4.1 Shukurani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa shughuli zake kwa kipindi cha Januari 2016 hadi Januari, 2017. Ni imani ya Kamati kuwa fursa hii inayotokana na masharti ya Kanuni ya 117 (15), ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, itasaidia kuliwezesha Bunge lako Tukufu kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia Serikali ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba, (Mb), Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi, (Mb) na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga, (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Angela Kairuki (Mb), na watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake.


**Mheshimiwa Spika**, Mwisho, lakini si kwa umuhimu, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas Kashillillah, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Aidha, nawashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Issa, Bi. Grace Bidya na Ndg. Hamisi Mwinyimkuu wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vema shughuli za Kamati kwa kipindi chote na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.



## 4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa, Uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, Maoni na Mapendekezo sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.



Balazi Asadi Mohamed Rajabu, Mb

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

10 Februari, 2017

**ORODHA YA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 NA  
KUKAGULIWA NA KAMATI YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA MWEZI MACHI/JUNI 2016**

<b>SN</b>	<b>WIZARA/ IDARA</b>	<b>SIMBO YA MRADI</b>	<b>FUNGU</b>	<b>KIFUNGU</b>	<b>JINA LA MRADI</b>	<b>MAHALI ULIPO</b>
<b>1.</b>	<b>Wizaraya Mambo yaNje, UshirikianowaAfrikaMasha riki, KikandanaKitaifa</b>	6391	34	1004	Ukarabatiwajengo la OfisinaMakaziyaBaloziinaM kuuwaUtawala	Maputo- Msumbiji
		6391	34	1004	UkarabatiwamakaziyaBalo zi	Stockholm, Sweden
<b>2.</b>	<b>Wizaraya Mambo yaNdani- Magereza</b>	4428	29	4003	Kuboreshamashambayam ifugo	Kinglwira, Morogoro King'ang'a, Dodoma
		6306	29	4001	Ukamilishajiwamajengoya Gereza	Segerea, Dar es Salaam
		6307	29	4001	Ukamilishajiwanyumbaza askari	Mkoka, Dodoma Kiomboi, Singida
		6308	29	4001	Kukarabatimajengonamiu ndombinuyamagerezayen yeulinzimkali	Isanga, Dodoma Segerea, Dar es Salaam
<b>3.</b>	<b>Wizaraya Mambo yaNdani-</b>	6301	93	2002	UkamilishajiuNyumbata	Dar es Salaam

	Uhamiaji					nozawatumishi	
4.	Wizaraya yaNdaniyaNchi Mambo	6339	93	2002	2002	KukarabatiJengo MakaoMakuuyaUhamiaji la	Dar es Salaam
		6327	51	1003	1003	UjenzinaUkarabatiwamaje ngoyaOfisi	Dar es Salaam
5.	Wizaraya Ulinzi naJeshi la KujengaTaifa	6501	51	1003	1003	VitambulishovyaTaifa	Dar es Salaam
		6103	57	1009	1009	Kuimarishamawasilianosol amaJeshini	Dar es Salaam
		6103	57	2001	2001	Ujenzinaukamilishajiwami undombinunakuendeleza uzalishajikatikaShirika la Mzinga	Morogoro
		6103	57	2004	2004	Ulipajiwafidianakupimam aeneoyaliyochukuliwakwa matumiziyaJeshi	

**TAARIFA YA UJUMBE WA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
KWENYE MKUTANO WA 134 WA UMOJA WA MABUNGE DUNIANI (IPU)  
LUSAKA, ZAMBIA 19 – 23 MACHI, 2016**

**1.0 UTANGULIZI**

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwanachama wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU). Hivyo, Bunge limekuwa likiwakilishwa kwenye Mkutano Mkuu (General Assembly), Semina, Warsha na makongamano mbalimbali yanayoandaliwa na Umoja huu. Mkutano Mkuu (Plenary Assembly) wa Umoja huu hufanyika mara mbili kwa mwaka. Mkutano Mkuu wa Mwezi Machi/Aprili hufanyika kwenye moja wapo ya Nchi Mwanachama na ule wa Mwezi Oktoba mara nyingi hufanyika kwenye makao makuu ya Umoja huu yaliyopo Geneva, Switzerland.

**2.0 UWAKILISHI WA BUNGE LA TANZANIA KWENYE MKUTANO WA 134**

Kwa mujibu wa Katiba ya Umoja wa Mabunge Duniani, Mabunge ya Nchi Wanachama huwakilishwa kwenye Mikutano wake mkuu kwa kuzingatia Idadi ya watu wa Nchi husika. Hivyo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huwakilishwa na Wajumbe sita Wajumbe ambao walichaguliwa na Bunge kwenye Mkutano wake wa pili. Wajumbe hao ni hawa wafuatao;

1. Mhe. Peter Serukamba (Mb)
2. Mhe. Suzan Lyimo (Mb)
3. Mhe. Pudenciana Kikwembe (Mb)
4. Mhe. Juma Othman (Mb)
5. Mhe. Mohamed Mchengelwa (Mb)

Aidha Mhe. Job Yustino Ndugai (Mb) Spika wa Bunge ndiye kiongozi wa Ujumbe wa Tanzania kwenye Mkutano wa IPU.

**3.0 USHIRIKI WA UJUMBE WA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWENYE MKUTANO WA 134, LUSAKA ZAMBIA**

Mkutano wa 134 wa IPU ulikuwa wa kwanza kuhudhuriwa na Wajumbe wetu tangu tulipochaguliwa mnamo mwezi Februari, 2016. Mkutano huu ulihudhuriwa na Wajumbe wote watano waliorodheshwa hapo juu. Aidha Mhe. Peter Serukamba (Mb) aliteuliwa kuongoza Ujumbe wuu kwa niaba ya

Mhe. Spika. Mbali na Mkutano Mkuu, Umoja wa Mabunge Duniani uliandaa Mkutano wa tatu wa Wabunge vijana, (The Third Forum of Young Parliamentarians of IPU), Mkutano wa masuala ya Ukimwi (Advisory Group on HIV/AIDS and Maternal, Newborn and child Health), Mkutano wa Makatibu wa Mabunge (Association of Secretaries General of Parliaments meeting) pamoja na Mkutano wa Wabunge wote wanawake (Meeting of women Parliamentarians).

Mikutano hii ilifanyika sambamba na Mkutano Mkuu na ilihudhuriwa na Wajumbe kutoka Bunge letu.

#### **4.0 MASUALA MAHSUSI YALIYOJITOKEZA KWENYE MKUTANO WA 134 WA MABUNGE DUNIANI**

Mkutano wa 134 ulifunguliwa rasmi mnamo tarehe 19 Machi, 2016. Kama Iliyo ada Mgeni Rasmi kwenye sherehe za ufunguzi alikuwa Mhe. Edgar Chagwa Lungua, Rais wa Jamhuri ya Zambia. Aidha, Spika wa Bunge la Zambia Mhe. Patrick Matibini alitoa hotuba ya ukaribisho. Vilelvile, Rais wa IPU Mhe. Saber Chowdhury pia alihutubia Wajumbe wakati wa Sherehe za ufunguzi wa Mkutano. Viongozi hawa watatu walisisitiza umuhimu wa Wajumbe kutoa kipaumbele zaidi kwa vijana ili waweze kutoa mchango wao katika maendeleo ya nchi zao kiuchumi, kijamii , kiutamaduni na kisiasa. Hotuba zao zilijikita kwenye mada kuu (theme) ya Mkutano wa 134 ambayo ni "Rejuvenating Democracy: giving voice to the Youth".

#### **5.0 MIJADALA KWENYE KAMATI MBALIMBALI ZA IPU**

Mkutano wa 134 ulitanguliwa na Mikutano ya Kamati mbalimbali za Umoja huo. Mkutano ya Kamati ilianza tarehe 16 -19 Machi, 2016 Kamati hizo ni hizi zifuatazo:-

- (i) Kamati ya amani na usalama wa kimataifa (Committee on peace and International Security)
- (ii) Kamati ya Masuala ya Umoja wa Mataifa (Committee on United Nations)
- (iii) Kamati ya Demokrasia na Haki za Binadamu (Committee on Democracy and Human Rights)

- (iv) Kamati ya Maendeleo Endelevu, Fedha na Biashara (Committee on Sustainable Development, Finance and Trade)

Kamati hizi ziliwasilisha rasimu za maazimio (draft resolutions) na mapendekezo kwa ajili ya kuridhiwa na Mkutano Mkuu.

## **6.0 MJADALA KUHUSU MASUALA YA DHARURA**

Kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha katiba ya IPU Nchi wanachama zinapaswa kuwasilisha suala lolote la dharura ili liweze kujadiliwa na Mkutano mkuu. Hadi kufikia tarehe 20 Machi, 2016 Nchi za Morocco, Sudan, Uruguay na Ufaransa zili timiza masharti ya nchi na kuwasilisha masuala ya dharura yafuatayo:-

- (i) Completing the process of International Recognition of a viable Independent and sovereign state with East Jerusalem as its capital: the Role of Parliaments (Morocco).
- (ii) Human Trafficking: an Act of Terrorism: a grave Violation of Human Rights and Human Dignity and Threat to regional and International Peace and security (Sudan).
- (iii) Parliamentary powers in democracies and the importance of the oversight function (Venezuela).
- (iv) Giving an identity to the 230 million children without a civil status: one of the major challenges of the humanitarian crisis in the 21<sup>st</sup> century (France and Uruguay).

Hata hivyo, Mabunge ya Nchi za Morocco na Venezuela yaliondoa maazimio yao kabla ya kupigiwa kura. Hivyo Baraza kuu (General Assembly) liliendesha mchakato wa kura kwa maazimio mawili yaliyosalia hatimaye azimio lililowasilishwa na nchi za Ufaransa na Uruguay lilipitishwa rasmi na kuwasilishwa kwenye Kamati ya Uandishi. Mkutano mkuu ulilijadili kwa kina Azimio hilo na kuliridhia rasmi mnamo tarehe 22 Machi, 2016.

## **7.0 MJADALA KUHUSU MADA KUU YA MKUTANO (REJUVINATING DEMOCRACY: GIVING VOICE TO THE YOUTH)**

Wajumbe kutoka Mabunge mbalimbali walitoa Michango yao kuhusu mada kuu ya Mkutano iliyoainishwa hapo juu. Jumla ya Wajumbe 95 walishiriki

kwenye mjadala huo kuhusu njia mbalimbali za kuwawezesha vijana kushiriki ipasavyo kwenye masuala ya kiuchumi na kisiasa. Bunge la Tanzania Mhe. Peter Serukamba alipata fursa ya kuchangia kwenye mjadala huu. Hotuba yake fupi imeambatanishwa na taarifa hii.

## **8.0 WATU MASHUHURI WALIOHUTUBIA BARAZA KUU LA IPU**

Mikutano mkuu ya IPU huwakanisha Wajumbe na watu mashuhuri duniani ambao hualikwa kuzungumzia masuala mahsusi. Mkutano wa 134 wa IPU uliwaalika watu mashuhuri wafuatao:-

- (i) Bw. A. Alhendawi – Mwakilishi wa katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Masuala ya Vijana.
- (ii) Bi. Yvonne Chaka chaka – Msanii na Balozi wa Umoja wa Mataifa wa kutokomeza Malaria
- (iii) Bw. V. Nayak mwanafunzi kijana aliyesaidia kampeni za Rais wa Marekani Mhe. Obama Mwaka 2012.

## **9.0 MAPENDEKEZO**

Kwa kuwa Mkutano wa 134 ulikuwa wa kwanza baada ya uchaguzi wa Wajumbe wa IPU kutoka Tanzania tunapenda kutoa mapendekezo yafuatayo ili kuboresha ushiriki wetu kwenye Mikutano hii kwa siku zijazo:-

- (i) Uwepo utaratibu wa wajumbe kukutana kabla ya kila Mkutano ili kuafikiana juu ya masuala muhimu yatakayojadiliwa.
- (ii) Ujumbe wa Bunge letu uwasili mapema kwenye Mkutano ili kushiriki Kwenye Mkutano wa kikanda wa Afrika (Africa geopolitical group) na hivyo kupata fursa ya kushiriki chaguzi za kujaza nafasi mbalimbali kwenye Kamati za IPU.
- (iii) Afisa Dawati kwa kushirikiana na wadau mbalimbali atayarishe “background papers” kuhusu mada mbalimbali zitakazojadiliwa kwenye Mkutano husika.
- (iv) Ujumbe wezeshwa ipasavyo hususan kupatiwa fedha za tahadhari ili kugharamia dharura kwa Wajumbe pale ambapo mazingira yanaleta changamoto.

- (V) Sekretarieti iandae vipeperushi vyenye picha za Wajumbe wa Bunge letu pamoja na Ukumbi wa Bunge, tovuti na anuani ya Bunge kwa ajili ya kugawiwa kwa Wajumbe wa Mkutano kutoka Nchi nyingine. Hatua hii itasaidia ubadilishanaji wa taarifa muhimu na Mabunge ya Nchi nyingine.

## 10. HITIMISHO

Mhe. Spika, napenda kuhitimisha kwa kukushukuru, kwa naiaba ya Wajumbe wenzangu kwa ushirikiano na imani kubwa uliyotupa. Tunapenda kukuahidi kuwa tutajituma kutekeleza kwa ufanisi wajibu wetu kwenye Mikutano na matukio mbalimbali ya chombo hiki muhimu.

Naomba kuwasilisha.



Mhe. Peter Serukamba (Mb)

**Kiongozi wa Ujumbe**

**28 JUNI, 2016**



## **TAARIFA YA SHUGHULI ZA BUNGE LA AFRIKA KUANZIA MWEZI MEI HADI AGOSTI, 2016**

### **1.0. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Nyongeza ya Nane Sehemu ya Pili kifungu 7(2) (a) (iii) Toleo la Mwaka 2016 na kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika, kutoka Bunge la Tanzania, napenda kuwasilisha taarifa hii ya Kwanza ya shughuli za Bunge la Afrika toka kuchaguliwa kwetu tarehe 26 Februari, 2016 kuwa wabunge wa Bunge la Afrika. Taarifa hii ya kwanza ni ya kuanzia mwezi Mei hadi Agosti, 2016.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe mwenyewe kwa kutupa nafasi hii kwa mara ya kwanza ili tuweze kuwasilisha taarifa ya shughuli za Bunge la Afrika kuanzia mwezi Mei hadi Agosti, 2016. Katika taarifa hii ya kwanza toka kuchaguliwa kwetu nitaeleza kwa kifupi kuhusu Muundo wa Bunge la Afrika, Mamlaka ya Bunge la Afrika, historia fupi ya Bunge la Afrika na shughuli muhimu zilizofanyika katika Bunge la Afrika kuanzia mwezi Mei hadi Agosti, 2016.

### **1.1. Wajumbe wa Bunge la Afrika Kutoka Bunge la Tanzania**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, abla ya kuwasilisha taarifa hii niruhusu kwanza niwatambue waheshimiwa wajumbe wa Bunge la Afrika kama ifuatavyo;

- i. Mhe. Dr. Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, Mwenyekiti wa Wabunge wa Bunge la Afrika.
- ii. Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mbunge wa Jimbo la Handeni Vijijini, Mjumbe

- iii. Mhe. Stephen Julius Masele, Mbunge wa Shinyanga Mjini, Mjumbe
- iv. Mhe. Asha Abdullah Juma, Mbunge Viti Maalum, Mjumbe
- v. Mhe. David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba, Mjumbe

## 1.2. Muundo wa Bunge la Afrika.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa kifupi kabisa, Bunge la Afrika limeundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 17 cha Mkataba wa Umoja wa Afrika (*Constitutive Act of the African Union*) ambapo mpaka sasa nchi 51 zimeridhia Mkataba huo. Kifungu cha 2 cha Itifaki inayounda Bunge la Afrika imeelezea uanzishwaji wa Bunge la Afrika na namna ya kuwapata Wabunge wake. Kwa mujibu wa Itifaki hiyo kila Bunge linabidi lichague Wabunge 5 na kati ya Wabunge hao lazima awepo angalau mbunge mmoja mwanamke na kwenye mabunge yenye vyama vingi pawe na uwakilishi wa vyama vya upinzani na hivyo uwakilishi wa Bunge la Afrika lazima utoe taswira ya Bunge la nchi husika mwanachama wa Umoja wa Afrika.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Itifaki hiyo pia imeelezea malengo na majukumu ya Bunge la Afrika, uchaguzi wa viongozi wake, utungaji wa kanuni zake, utendaji kazi katika vikao vyake, mahusiano na vyombo mbalimbali na utaratibu wa kufanya marekebisho katika Itifaki hiyo. Bunge la Afrika ni moja ya taasisi Kumi za Umoja wa Afrika.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Malengo ya kuanzishwa kwa Bunge la Afrika ni kurahisisha uhimizaji wa utekelezaji bora wa sera, kanuni na taratibu zilizowekwa na Umoja wa Afrika kwa manufaa ya bara la Afrika, kuhamasisha nchi kufuata haki za binadamu,

utawala wa sheria na uwajibikaji, kuimarisha amani, ulinzi na usalama na kuboresha njia za ushirikiano katika bara la Afrika. Kuwaelimisha wananchi katika nchi za Afrika kuhusu malengo na sera ambazo zitasaidia kuunganisha waafrika wote kwa lengo la kuleta maendeleo kwa njia ya kujitegemea na kujenga uchumi endelevu. Kuweka mbinu za kuleta ushirikiano na maendeleo ya Afrika, kuimarisha Umoja wa bara la Afrika na kujenga mwelekeo mmoja miongoni mwa watu wa Afrika na kuleta ushirikiano miongoni mwa maeneo ya Jumuiya za kiuchumi na mabunge yao.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa kuwakumbusha tu, Bunge la Afrika lilizinduliwa rasmi Addis Ababa, Ethiopia tarehe 18 Machi, 2004, na Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika aliyechaguliwa alikuwa Mhe. Dkt. Gertrude Ibengwe Mongela aliyekuwa Mbunge wa Ukerewe kutoka Bunge la Tanzania. Katika Bunge la Afrika, kiongozi wa juu wa taasisi hiyo ni Rais wa Bunge la Afrika, Rais anasaidiwa na Makamu wa Rais wanne mmoja kutoka katika kila Kanda na kati ya hao lazima mmoja wapo awe mwanamke. Rais na Makamu wake wanne wa Bunge la Afrika wanaunda Kamati ya Uongozi yaani *Bureau Members*.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Katika kutekeleza shughuli zake Kamati ya Uongozi ya Bunge la Afrika inasaidiwa na Sekretarieti ya Bunge la Afrika ambapo Sekretarieti hiyo inaongozwa na Katibu wa Bunge la Afrika akisaidiwa na Naibu Katibu wa Bunge wawili. Katibu wa Bunge wa sasa ni kutoka Algeria, Naibu Katibu wa Bunge mmoja ni kutoka Gambia na wa pili ni kutoka nchini Sudan.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, aidha kuna idara na vitengo mbalimbali katika kulisaidia Bunge la Afrika kufanya kazi zake kwa ufanisi. Kila

Kanda (Kati, Kusini, Mashariki, Magharibi na Kaskazini) inaunda Umoja wake yaani (*Regional Caucus*). Kanda hizo zinashughulikia masuala mbalimbali yanayohusu maslahi ya kanda hizo ikiwa ni pamoja na kupendekeza na kuteua wajumbe watakao wakilisha kanda katika Kamati za kudumu za Bunge la Afrika, inapendekeza wabunge wanaoomba kugombea uongozi katika Kamati, kugombea uongozi wa Umakamu Rais na Urais na masuala mengine yahasuyo ustawi wa kanda katika Afrika.

### **1.3. Vikao vya Kamati na Mikutano ya Bunge la Afrika**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika utendaji kazi wa Bunge la Afrika kazi nyingi zinafanyika katika vikao vya Kamati na mikutano ya Bunge. Kuanzia mwezi Mei hadi Agosti, 2016, wabunge wa Bunge la Afrika wamehudhuria vikao vya Kamati mara moja na Mikutano wa Bunge la Afrika mara moja kama ifuatavyo:-

- Mikutano wa Pili wa Bunge la Nne wa Bunge la Afrika uliofanyika tarehe 29 Aprili hadi 13 Mei, 2016, Midrand, Afrika ya Kusini.
- Vikao vya Kamati za Bunge la Afrika vilivyofanyikakuanzia 28 Julai hadi 5 Agosti, 2016, Midrand Afrika ya Kusini

### **1.4. Lugha Zinazotumika Katika Bunge la Afrika**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa kifupi napenda kuwakumbusha kwamba kwa mujibu wa Mkataba wa Umoja wa Afrika na Itifaki iliyounda Bunge la Afrika na pia kwa mujibu wa Kanuni za Bunge la Afrika lugha zinazotumika katika Mikutano ya Bunge la Afrika ni tano nazo ni; Kiswahili, Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu na Kireno.

### **1.5. Makao Makuu ya Bunge la Afrika**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, makao makuu ya Bunge la Afrika yapo nchini Afrika ya Kusini, uteuzi wa kuifanya nchi ya Afrika ya Kusini kuwa Makao Makuu ya Bunge la Afrika yalifanywa na Wakuu wa

nchi (Marais) wa Umoja wa Afrika mwaka 2004. Vikao vya Kamati na Mikutano ya Bunge la Afrika mara nyingi inafanyika katika nchi ya Afrika ya Kusini. Hata hivyo nchi nyingine yeyote ya bara la Afrika inaweza kuomba vikao vya Kamati au Mikutano ya Bunge la Afrika kufanyika katika nchi hiyo baada ya kuridhiwa na Bunge la Afrika.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, toka Bunge la Afrika lizinduliwe mwaka 2004, Mktano mmoja tu umewahi kufanyika Addis Ababa, nchini Ethiopia Januari, 2012. Hata hivyo mwaka huu 2016 nchi ya Misri imeomba mkutano wa Bunge la Afrika unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba utakaofanyika nchini Misri, bunge la Afrika tayari limeridhia ombi hilo. Hata sisi Tanzania wakati muafaka ukifika kupitia Kamati yako Mwenyekiti tutaomba Bunge la Afrika lifanyike hapa Dodoma, nchini Tanzania.

## **2.0. MAMBO MUHIMU YALIYOFANYIKA KATIKA KIPINDI CHA KUANZIA MWEZI MEI HADI AGOSTI, 2016**

### **2.1. KUJADILI MIGOGORO BARANI AFRIKA**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Katika kipindi chetu kifupi wakati wa vikao vya Kamati za Bunge la Afrika na Mkutano wa Bunge la Afrika tulijadili kwa kina kuhusu masuala ya Amani na Usalama katika Bara la Afrika, taarifa mbalimbali ziliwasilishwa na watendaji wakuu wa Umoja wa Afrika kuhusu namna Umoja wa Afrika unavyoshughulika suala la migogoro barani Afrika. Hii ni Kutokana na umuhimu wa amani na usalama katika kuleta maendeleo katika nchi za Afrika.

#### **2.1.1. Mgogoro Nchini Burundi.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika Mkutano wa Pili wa Bunge la Nne, mwezi Mei, 2016 wabunge wa Bunge la Afrika walijadili mgogoro wa Burundi. Bunge la Afrika lilituma timu ya wabunge wa Bunge la

Afrika kwenda nchini Burundi kufanya uchunguzi ili kujua hali halisi ya mgogoro wa Burundi. Baada ya timu hiyo kukamilisha kazi yake na kuwasilisha taarifa Bungeni. Ilibainika kwamba mgogoro wa Burundi ulianza pale ambapo Rais Pierre Nkurunziza alipoamu kugombea urais kwa awamu ya tatu. Rais Nkurunziza alipata nguvu za kugombea baada ya Mahakama ya Katiba nchini Burundi kuamua kwamba awamu ya kwanza ya Rais Nkurunziza aliteuliwa na alichauguliwa na wabunge wa Bunge la Burundi na sio wananchi. Hivyo awamu ya Kwanza hakuchaguliwa na wananchi kutokana na ukweli huo Rais Nkurunziza anayo haki ya kugombea urais kwa awamu ya pili na sio awamu ya tatu.

**Mheshimiwa Mwenyekiti** kutokana na uamuzi wa Rais Nkurunziza kugombea urais kukazuka maandamano mbalimbali nchini Burundi hasa katika mji wa Bujumbura na miji mingine mikubwa. Aidha tarehe 13 Mei, 2015 lilifanyika jaribio la kuipindua Serikali ya Rais Nkurunziza, jaribio ambalo halikufanikiwa. Matokeo yake Serikali ikawakamata watu ambao walihusika katika mapinduzi hayo. Baada ya machafuko hayo na maandamano kuendelea taasisi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Umoja wa Afrika Mashariki na Umoja wa Afrika walianzisha mikakati ya kusuluhisha mgogoro wa Burundi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, uchunguzi wa timu iliyotumwa kwenda Burundi ulionyesha kwamba toka nchi ya Burundi ipate uhuru na baada ya Mkataba wa Arusha bado kuna changamoto nyingi zinazowakabiliwa wananchi wa Burundi changamoto ambazo bado hazijapatiwa ufumbuzi. Hivyo nchi ya Burundi bado ni tete katika masuala ya usalama na amani na kuna changamoto nyingi ambazo zimesababisha kutokuwepo na amani na usalama wa kudumu katika nchi hiyo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, baada ya majadiliano makubwa katika vikao vya Kamati na katika Bunge, Bunge la Afrika lilipendekeza kwamba ili kuondokana na mgogoro huo vyombo vya kimataifa Umoja wa Kimataifa, Umoja wa Afrika na Umoja wa Afrika ya Masharikiinabidi kuandaa jukwaa la majadiliano ili kutafuta ufumbuzi wa kudumu mgogoro wa Burundi ikiwa ni pamoja na kutatua changamoto za ndani ya Burundi.

### **2.1.2. Mapambano Dhidi ya Ugaidi Katika Bara la Afrika**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika Vikao vya Kamati vilivyofanyika mwezi Agosti, 2016, Midrand, Afrika ya Kusini, wabunge wa Bunge la Afrika wakiongozwa na Kamati ya Ushirikiano na Uhusiano wa Kimataifa na Utatuzi wa Migogoro walijadili kwa kina changamoto ya ugaidi katika bara la Afrika na mikakati ya kupambana na ugaidi. Lengo la mjadala huo ni kuwawezesha wabunge wa Bunge la Afrika kuelewa kwa kina suala la ugaidi na kuweza kuelewa mikakati iliyowekwa na Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Umoja wa Afrika, Umoja wa Kikanda ( EAC, ECOWAS, SADC) na mikakati, sheria na kanuni ya nchi moja moja katika kupambana na ugaidi katika bara la Afrika na duniani kwa ujumla.

### **2.2. Haki za Binadamu za Kuwalinda Wanawake**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika Mkutano wa Pili wa Bunge la Nne, wabunge wa Bunge la Afrika walijadili kwa kina haki za binadamu kwa ujumla na msisitizo mkubwa kwa haki zinazowahusu wanawake. Katika majadiliano hayo ilielezwa kwamba Mwaka 2003, wakuu wa nchi wa Umoja wa Afrika walisaini Itifaki ya Haki za Binadamuyenye lengo la kuendeleza na kulinda haki za wanawake katika bara la Afrika (*the Protocol to the African Charter on Human and People's Rights on the Rights of Women in*

*Africa*) Itifaki ambayo imeweka utaratibu wa kusimamia na kulinda maendeleo na haki za binadamu katika bara la Afrika. Hii ilikuwa ni hatua kubwa sana iliyofanywa na Umoja wa Afrika katika kuendeleza na kulinda haki za wanawake barani Afrika.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, aidha, kwa mujibu wa ripoti ya IPU, takwimu zinaonyesha kwamba idadi ya wanawake katika vyombo vya maamuzi zinazidi kuongezeka duniani, mwaka 1995 duniani kulikuwa na wanawake katika vyombo vya maamuzi asilimia 9.8 tu, mwaka 2005 asilimia 14.5, mwaka 2015 asilimia 22.3 na kuliweka bara la Afrika katika nafasi ya tatu kati ya mabara yote sita(6). Hata hivyo takwimu zinaonyesha kwamba nchi ya Rwanda katika Bunge ina asilimia 64 na kuifanya kuwa nchi ya kwanza duniani kuwa na asilimia kubwa ya wanawake katika Bunge. Nchi zingine ambazo zina asilimia kubwa ya wanawake katika Bunge ni kama vile Afrika ya Kusini, Tanzania, Cape Verde na Lesotho nchi hizo zina idadi ya zaidi ya asilimia 30 katika mabunge yao.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, pamoja na kwamba takwimu nyingi zinaonyesha kwamba kuna zaidi ya asilimia 50 ya idadi ya wanawake katika Afrika na hata hapa Tanzania, lakini wanawake bado wanakabiliwa na unyanyasaji wa kijinsia, mila potofu, bado kuna tatizo la kurithi ardhi, ubakaji na madhara yatokanayo na vita. Wanawake wanakabiliwa na ukosefu wa ajira, kutokuwa na elimu na huduma hafifu za afya.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, wabunge wa Bunge la Afrika la Afrika baada ya kujadili kwa kina suala la haki za binadamu kwa wanawake walipendekeza kwamba mabunge yetu ya nchi zitunge sheria mpya au kuzifanyia marekebisho sheria ambazo zimepitwa na wakati ili kuweka mikakati ya kuwalinda wanawake



na watoto katika maeneo mbalimbali hasa kuondoa unyanyasaji wa kijinsia, kuondoa mila potofu na kuweka mikakati ya kuendeleza wanawake na watoto. Hata hivyo Bunge letu na Serikaliimepiga hatua kubwa katika suala la kutunga sheria mpya na kuzifanyia marekebisho sheria zilizopitwa na wakati katika kuwalinda wanawake na watoto.

### **2.3. Kujadili Changamoto Zinazokabili Sekta ya Sayansi, Teknolojia, Ufundi na Elimu Barani Afrika**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, wabunge wa Bunge la Afrika katika Mkutano wa Pili wa Bunge la Nne uliofanyika mwezi Mei, 2016, wabunge walijadili kwa kina changamoto zinazokabili sekta ya sayansi, teknolojia, ufundi na elimu katika bara la Afrika. Taarifa mbalimbali zilizowasilishwa zinaonyesha kwamba bara la Afrika limesaini Itifaki na protokali kadhaa zinazolenga kuboresha sekta ya Sayansi, teknolojia, ufundi na elimu barani Afrika, lakini bado juhudi hizo hazijaleta mafanikio makubwa katika bara la Afrika ukilinganisha na mabara mengine hasa katika nchi zilizoendelea. Sababu kubwa zinazotajwa za kutokuwa na maendeleo makubwa katika sekta hizo ni pamoja na kutokuwa na utashi wa dhati wa kisiasa, ukosefu wa fedha za kutosha na maandalizi hafifu ya jamii katika kuendeleza sekta hizo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, wabunge baada ya kujadili changamoto mbalimbali walipendekeza kwamba viongozi wa nchi zetu wawe na utashi wa dhati katika kuendeleza sekta hizo muhimu sana kwa maendeleo ya nchi zetu. Viongozi wetu waweke mikakati na mazingira mazuri ya kuboresha mazingira katika kuendeleza sekta hizo, kuwaenzi wataalam wetu ili wasikimbie nchi na kwenda nchi zingine (*reverse brain drain*). Kuna umuhimu wa kuandaa vijana kuwa wabunifu wa kazi

badala ya kuwaandaa kuwa waombaji wa kazi (*job creator rather than job applicants*).

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, aidha, ilipendekezwa kwamba kuna umuhimu wa kuendeleza sekta ya elimu, sayansi, teknolojia na ufundi kwa kujenga ushirikiano wa pamoja katika bara la Afrika, kujenga utawala bora katika kuendesha shughuli hizo, viongozi waweke mikakati ya kuendeleza sayansi, elimu ya ufundi na hesabu. Kujenga misingi imara ya mifumo ya ufundishaji, ukusanyaji wa takwimu na uchambuzi wa takwimu kiutaalam.

#### **2.4. Kujadili Hali ya Usalama wa Chakula na Lishe Barani Afrika**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika Mkutano wa Pili wa Bunge la Nne, wabunge wa Bunge la Afrika walijadili kwa kina suala la hali ya usalama wa chakula na lishe barani Afrika. Takwimu za Shirika la Chakula Duniani (FAO) za mwaka 2015 zinaonyesha kwamba zaidi ya watu 793 milioni duniani wanakabiliwa na njaa na lishe duni. Baada ya majadiliano ya kina ilipendekezwa kwamba ili kupambana na uhaba wa chakula na tatizo la lishe barani Afrika, wabunge katika nchi mbalimbali lazima waweke mikakati ya kuboresha sheria zinazohusiana na chakula na lishe, kutoa kipaumbele katika bajeti ya kilimo na njia bora za kuisimamia sekta ya kilimo hasa suala la chakula na lishe.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika kupambana na changamoto za chakula, lishe na umaskini barani Afrika, mabunge yetu ya Afrika, Bunge la Ulaya na Shirika la Chakula Duniani (FAO) washirikiane katika kuandaa sera, sheria na mikakati madhubuti katika kushughulikia changamoto hizo. Ni muhimu kuwa na chombo maalum cha kushughulikia suala la chakula, lishe na umaskini. FAO iweke mikakati ya kukusanya taarifa, sera na mifumo bora katika nchi mbalimbali (*best practice*) ili kuweza

kujadiliana na kupendekeza namna bora ya kushughulikia suala la chakula, lishe na umaskini barani Afrika.

## **2.5. Kujadili Namna Bora ya Kuendeleza Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika Bara la Afrika**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika Mkutano wa Pili wa Bunge la nne wabunge wa Bunge la Afrika walijadili namna bora ya kuendeleza TEHAMA na ya kutatua changamoto zake katika bara la Afrika. Ni ukweli kwamba katika ulimwengu wa sasa wa utandawazi maendeleo ya dhati yanategemea sana ujuzi na weledi katika masuala ya TEHAMA. Ukweli ni kwamba watu wote sasa tunaishi katika dunia ya teknolojia ya habari na mawasiliano ambapo kila mdau ni muhimu kuelewa elimu hiyo ili kila mtu aweze kuishi maisha ya maendeleo inabidi awe na ujuzi wa TEHAMA. Nchi zetu za kiafrika hazina budi kuweka mikakati ya kuendeleza elimu ya TEHAMA katika ngazi zote za maisha kuanzia shule za awali, msingi, sekondari na elimu ya juu

## **2.6. Kujadili Mikakati ya Kuridhia Itifaki na Mikataba Mbalimbali Zilizopitishwa na Umoja wa Afrika hasa Itifaki inayounda Bunge la Afrika (*Reviewed Protocol Relating to the Pan-African Parliament*)**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, baada ya kazi kubwa ya kupitishwa kwa Marekebisho ya Itifaki iliyounda Bunge la Afrika mwezi Juni, 2014, Malabo, nchini Guinea, kazi kubwa ambayo imebaki kufanywa na Bunge la Afrika ni kuweka mikakati ya namna ya haraka ya kuridhia Itifaki hiyo na Mikataba mingine iliyopitishwa na Umoja wa Afrika.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika Mkutano wa Pili wa Bunge la nne uliofanyika mwezi Mei, 2016 na katika vikao vya Kamati za Bunge la Afrika vilivyofanyika mwezi Agosti, 2016, Midrand, Afrika ya Kusini, wabunge walijadili mikakati mbalimbali ya namna bora ya

kuhamasisha mabunge yetu kuridhia kwa haraka Itifaki iliyounda Bunge la Afrika. Wabunge wa Bunge la Afrika pamoja na mikakati mingine walikubaliana kwamba ni muhimu kwa mabunge ya nchi yetu kwa kushirikiana na Serikali kuandaa mikutano na vikao vya kujadili namna ya kuridhia kwa haraka Itifaki na mikataba mbalimbali iliyopitishwa na Umoja wa Afrika kwa lengo la kuharakisha maendeleo na ustawi wa jamii barani Afrika.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika Vikao vya Kamati za Bunge la Afrika vilivyofanyika mwezi Agosti, 2016, Midrand, Afrika ya Kusini, Rais wa Bunge la Afrika aliwaalika Maspika na Makatibu wa Bunge kutoka katika nchi zote za Umoja wa Afrika. Lengo kubwa ikiwa ni kujadili mwenendo wa uridhaji wa mikataba na Itifaki zilizopitishwa na Umoja wa Afrika hasa Itifaki inayounda Bunge la Afrika. Kujadili changamoto zinazohusiana na kazi ya kuridhia itifaki na mikataba hiyo na mikakati bora ya kuigwa ya utekelezaji wa mikataba iliyopitishwa na Umoja wa Afrika (best practice).

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika Mkutano wa Makatibu wa Bunge uliofanyika tarehe 3 Agosti, 2016 na Mkutano wa Maspika uliofanyika tarehe 4-5 Agosti, 2016, Midrand, Afrika ya Kusini, walijadili faida ya kuridhia mikataba na itifaki zilizopitishwa na Umoja wa Afrika kwa nchi wanachama, Bunge la Afrika na kwa Umoja wa Afrika. Aidha walijadili mikakati mbalimbali ya namna bora ya kuharakisha uridhaji wa mikataba na Itifaki zilizopitishwa na Umoja wa Afrika.

## **2.7. Athari za Mabadiliko ya Tabia Nchi**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Katika Mkutano wa Pili wa Bunge la Nne wa Bunge la Afrika, wabunge walijadili kwa kina suala la athari za mabadiliko ya tabia nchi katika mazingira yetu, na kuangalia mikataba, maazimio ya kimataifa na mikakati ya nchi mojamoya

juu ya suala hili. Japokuwa nchi zinazoendelea ndizo zimechangia ongezeko la gesi ukaa kwenye anga kutoka kwenye viwanda vyao vinayoongeza joto duniani na kusababisha mabadiliko ya tabia nchi. Lakini Afrika inasemekana ndiyo itakumbwa na matatizo makubwa zaidi yanayotokana na athari hizo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, hali hii isipodhibitiwa, bara la Afrika litakumbwa na mafuriko, vipindi virefu vya ukame, vimbunga, sunami, maeneo yaliyo mabondeni na visiwa vidogo kumezwa na maji, njaa, umaskini na vita vitakavyotokana na kugombea raslimali ardhi na maji. Katika mikutano ijayo ya kujadili changamoto za athari za tabia nchi duniani, Bunge la Afrika linautaka Umoja wa Afrika kuweka mikakati madhubuti katika kushughulikia suala la athari za mabadiliko ya tabia nchi. Waheshimiwa wabunge, taasisi zisizo za kiserikali, Serikali, taasisi za kimataifa na wananchi kwa ujumla wahusishwe kwa karibu kabisa na kwa ukamilifu katika kutafuta ufumbuzi wa mabadiliko ya tabia nchi.

## **2.8. Kujadili Bajeti ya Umoja wa Afrika ya Mwaka 2017**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika Mkutano wa Pili wa Bunge la Nne la Bunge la Afrika, wabunge walijadili bajeti ya mwaka 2017 ya Umoja wa Afrika na taasisi zake. Bajeti iliyowasilishwa na Ndg. Erastus Mwencha Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika. Jumla ya Bajeti yote ya Umoja wa Afrika kwa mwaka 2017 ni dola za kimarekani 781,606,122. Ikiwa bajeti ya matumizi ya kawida ni dola za kimarekani 493,075,789 sawa na 63% na matumizi ya Miradi ya Maendeleo ni kiasi cha dola za kimarekani 288,530,333 sawa na 37%.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, maeneo muhimu yaliyopewa kipaumbele katika bajeti ya mwaka 2017 ni pamoja na kujenga uwezo katika sekta zinazohusu zaidi maendeleo ya wanawake na watoto, kuendeleza amani na usalama barani Afrika ikiwa ni pamoja na kupambana na ugaidi. Aidha kwa upande wa miradi ya maendeleo kipaumbele kimetolewa kwa ujenzi wa miundombinu hasa treni ya kisasa (*integrated High Speed Train Network*), ujenzi wa mifumo bora ya elimu katika vyuo vikuu katika bara la Afrika na kuendeleza namna bora ya matumizi ya raslimali zilizopo katika bara la Afrika (*Natural Resources Management*)

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2017, Bunge la Afrika limepangiwa kutumia kiasi cha dola za kimarekani 23,421,097. Fedha hizo zitatumika hasa katika uendeshaji wa shughuli za mikutano ya Bunge la Afrika na Kamati zake. Aidha, baadhi ya fedha zitatumika katika kulipa mishahara ya watumishi wa Bunge la Afrika na maendeleo ya watumishi wa Bunge hilo ikiwa ni pamoja na kuwaandaa watumishi katika Bunge la kutunga sheria na namna bora ya kulitangaza Bunge la Afrika katika ngazi ya chini hasa kwa wananchi wa kawaida.

## **2.9. Kujadili Changamoto Zinazokabili Biashara katika Bara la Afrika**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, biashara ni sekta muhimu sana katika maendeleo ya bara la Afrika, lakini bara la Afrika kibiashara linakabiliwa na changamoto nyingi sana kuliko mabara mengine yote. Ili kufanikisha biashara katika bara la Afrika, Bunge la Afrika kwa kushirikiana na mabunge ya nchi za Afrika hazina budi kuweka mikakati ya kurekebisha sheria na sera mbalimbali zinazozuia kushamiri kwa biashara katika bara la Afrika. Bunge la Afrika na mabunge ya nchi za Afrika ziweke mikakati ya kuridhia

itifaki na mikataba yote itakayosaidia kutatua changamoto za biashara katika bara la Afrika.

## **2.10. Mikakati ya Kujadili Namna Bora ya Kupambana na Rushwa Barani Afrika**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika Mkutano wa Pili wa Bunge la Nne, wabunge wengi wa Bunge la Afrika walibaini kwamba chanzo kikubwa cha umaskini na maendeleo duni katika bara la Afrika ni rushwa hasa rusha kubwa kubwa zinazofanywa na viongozi wa serikali na taasisi za umma barani Afrika. Ili kupambana na rushwa ya namna hiyo mikakati imara na bora lazima iandaliwe. Bunge la Afrika na mabunge ya nchi za kiafrika ni muhimu kusimamia kwa karibu serikali zetu kuhusiana na vita ya kupambana na rushwa na hasa taasisi zinazohusiana na mapambano ya rushwa ikiwa ni pamoja na taasisi zisizo za kiserikali.

## **2.11. Namna Bora ya Kusismamia Taasisi za Umoja wa Afrika na utaratibu wa Kupitisha Sheria ya Mifano(Model Laws).**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, hivi karibuni, Bunge la Afrika litakuwa ni chombo cha kutunga sheria ya mfano na kuboresha usimamizi wa taasisi za Umoja wa Afrika kwa maendeleo ya Umoja wa Afrika. Aidha, katika Itifaki iliyorekebishwa Bunge la Afrika litakuwa na uwezo wa kutunga sheria ya mfano kwa kuamua lenyewe au kwa kuagizwa na Umoja wa Afrika. Hivyo ni muhimu kwa wabunge wa Bunge la Afrika kuwa na uelewa mpana zaidi wa sera na namna ya kuandaa miswada ya sheria na kuzielewa taratibu bora za upitishwaji wa miswada ya sheria.

**2.12. Mikakati ya Uhamasishaji wa Kuridhia, Urasimishaji na Utekelezaji wa Itifaki na Mikataba iliyopishwa na Umoja wa Afrika**  
**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Bunge la Afrika limebaini kwamba katika bara la Afrika hakuna mikakati ya kutosha na ya dhati katika kuridhia, urasimishaji na kutekeleza itifaki na mikataba iliyopitishwa na Umoja wa Afrika. Wabunge wa Bunge la Afrika katika Vikao vyake vya Kamati vilivyofanyika mwezi Agosti, 2016 walijadili kwa kina namna bora ya kuhamasisha uridhiaji, urasimishaji na utekelezaji bora wa itifaki na mikataba inayopitishwa na Umoja wa Afrika.

### **3.0. CHANGAMOTO ZINAZOLIKABILI BUNGE LA AFRIKA**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Pamoja na mafanikio katika kutekeleza shughuli za Bunge la Afrika, pamekuwepo na changamoto mbalimbali katika Bunge la Afrika ambapo changamoto hizo zikitafutiwa ufumbuzi, Bunge la Afrika linaweza kufanyakazi nzuri kwa manufaa ya waafrika wote na maendeleo ya Jamii kwa ujumla

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, nitataja changamoto chache, Bunge la Afrika bado linakabiliwa na upungufu wa fedha za kuendesha shughuli za Bunge hasa pale ambapo hata bajeti iliyopitishwa na Bunge hilo fedha zake hazipatikani kwa maelezo kwamba baadhi ya nchi wanachama hazijatoa michango yao katika Umoja wa Afrika. Hii inasababisha maandalizi ya vikao vya Kamati na Mikutano ya Bunge la Afrika kukabiliwa na changamoto nyingi. Hadi sasa bado tatizo hili halijapatiwa ufumbuzi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, aidha kumekuwa na ushirikiano duni katika kutekeleza maamuzi, mapendekezo, ushauri na maoni kutoka katika Bunge la Afrika kwenda katika Umoja wa Afrika. Kumekuwa na tofauti kubwa sana katika uendeshaji wa shughuli



za kibunge kati ya nchi zinazotumia mila na desturi za kiingereza, kifaransa na kiarabu, hii ikiwa ni pamoja na changamoto ya lugha. Changamoto zingine ni pamoja na mabadiliko ya mara kwa mara ya wabunge wa Bunge la Afrika kutokana na wabunge kupoteza ubunge wao katika chaguzi katika nchi zao. Udhaifu wa Sekretarieti ya Bunge la Afrika hasa kwa kuwa na watumishi wachache na wenye uzoefu mdogo wa masuala ya kibunge.

#### **4.0. MAPENDEKEZO**

##### **4.1. Mapendekezo Kuhusu Namna ya Kutatua Migogoro katika Bara la Afrika hasa Mgogoro wa Burundi.**

1. Serikali zetu lazima ziimarishe uwekezaji katika sekta ambazo zinaweza kuibua ajira hasa kwa vijana. Serikali zetu ziwekeze katika sekta za maendeleo ya wananchi hasa elimu, afya, kuheshimu haki za binadamu na kuzingatia utawala bora.
2. Nchi wanachama wa Umoja wa Afrika zisaini na kuridhia mikataba yote inayohusiana na utatuzi wa migogoro. Viongozi wa nchi zetu wajifunze kutoka katika vurugu zilizosababisha Mapinduzi katika nchi za kiarabu. Kwa mgogoro wa Burundi taasisi za Umoja wa Afrika ya Mashariki na Umoja wa Afrika uharakishe kukaa na kujadili namna ya kutatua mgogoro huo

##### **4.2. Pendekezo kuhusu Kuridhia Itifaki na Mikataba Iliyopitishwa na Umoja wa Afrika hasa Itifaki Inayounda Bunge la Afrika**

1. *Mabunge ya nchi za Umoja wa Afrika ziharakishe mchakato wa kuridhia itifaki inayounda Bunge la Afrika ili kuharakisha Bunge la Afrika kuwa chombo cha kutunga sheria ili liweze kutunga sheria, kuandaa sera na mipango mbalimbali katika bara la Afrika.*

#### **4.3. Pendekezo Kuhusu Athari za Mabadiliko ya Tabia nchi.**

1. Watu wengi zaidi hasa wananchi wa kawaida, asasi zisizo za kiserikali, mabunge, washiriki katika kuhamasisha na kuelimisha jamii juu ya athari za mabadiliko ya tabia nchi. Kila nchi iwe na mpango mkakati wa kupunguza na kuzuia athari,
2. Nchi zilizoendelea watekeleze ahadi zao walizoweka za kuleta teknolojia ya kisasa kwenye mambo ya hali ya hewa, watoe wataalam na fedha za kuthibiti hali hii.

#### **5.0. SHUKRANI**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, tunatoa shukrani kwako, kwa Kamati yako, Waheshimiwa Wabunge wote wa Kamati yako kwa kutusikiliza. Tunaomba taarifa yetu hii ijadiliwe katika Kamati hii na ikiwezekana iwasilishwe katika Mkutano wa Bunge Februari, 2017, hapa Dodoma, ili kuwapa fursa nzuri waheshimiwa wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na watanzania wote kufuatilia shughuli za Bunge la Afrika.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, sisi kama wabunge wa Bunge la Afrika tunaomba kuimarisha ushirikiano wetu na Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, Kikandana Kimataifa kwa lengo la kufanya kazi zetu kwa ufanisi mkubwa zaidi. Tunaomba pia ushirikiano na Kamati yako ili tuweze kupata taarifa sahihi na hivyo kutuwezesha kuifanya kazi hii ya uwakilishi vizuri zaidi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, mwisho napenda kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Katibu wa Bunge kwa kutuwezesha wabunge wa Bunge la Afrika kufanya kazi zake. Aidha natoa shukrani za dhati kwa Katibu wa Wabunge wa Bunge la Afrika Ndugu Lawrence Robert Makigi kwa kutusaidia katika shughuli zote za Bunge la Afrika ikiwa ni pamoja na kuandaa rasimu ya taarifa hii.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, waheshimiwa wabunge, baada ya kusema hayo sasa ***Naomba Kuwasilisha Taarifa yetu.***



Dr. Faüstine Engelbert Ndugulile, MB

**MWENYEKITI WA WABUNGE WA BUNGE LA AFRIKA**

**Februari, 2017**

**MAELEZO YA WAWAKILISHI KWENYE JUKWAA LA KIBUNGE LA NCHI  
WANACHAMA WA JUMUIYA YA MAENDELEO YA KUSINI MWA AFRIKA  
(SADC-PF) KWA KIPINDI CHA JULAI – OKTOBA 2016**

**KWA AJILI YA KUWASILISHWA KWENYE KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE  
YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

**TAREHE 25 OKTOBA, 2016**

**DODOMA**

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa niaba ya Wawakilishi kwenye Jukwaa la Mabunge ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC- PF) naomba kuwasilisha maelezo mafupi kuhusu Jukwaa hili la Kibunge mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, kwa mujibu wa Kifungu cha 7(2) (3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, awali ya yote nianze kwa kutoa shukurani zetu za dhati kwa kupangwa kwenye ratiba ya kikao hiki ili tuwasilishe taarifa yetu kwa Kamati hii kama kanuni zinavyohitaji. Ni utaratibu mzuri unaoweza kuongeza tija katika uwakilishi wetu na pia kwa uanachama wetu katika Jukwaa la Jumuiya hii na pia katika Jumuiya ya SADC kwa ujumla. Baada ya kusema hayo, naomba sasa kwa ufupi kuelezea historia ya Jukwaa la Kibunge la nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC-PF).

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Jukwaa hili lilianzishwa mwaka 1997 Jijini Blantyre, Malawi kufuatia mkutano wa Wakuu wa nchi wanachama kukubali na kupitisha uwepo wa Jukwaa hilo (SADC PF ) kama moja ya Taasisi za SADC kwa mujibu wa kifungu cha 9(2)<sup>1</sup> cha Mkataba wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Madhumuni makubwa ya kuanzishwa kwa Jukwaa hili la kibunge ni kupata sehemu ambayo Mabunge na Wabunge kwa ujumla wa nchi wanachama wanaweza kubadilishana uzoefu na mawazo chanya ili kuimarisha mshikamano wa nchi husika kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Shabaha ya kuanzishwa kwa Jukwaa hilo kama ilivyodhihiri katika Mkutano wa Blantyre ni hatimaye kuwa na Bunge la Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC-PARLIAMENT*) kama ilivyo kwa kanda nyinginezo ambazo tayari zina Mabunge yao. Mfano wa Mabunge hayo ya Kanda ni Bunge la Afrika (PAP) na Bunge la Afrika Mashariki (EALA).

Kwa sasa nchi wanachama wa Jukwaa hili la Kibunge ni 14 ambazo ni: - Afrika ya Kusini, Angola, Botswana, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Lesotho, Malawi, Mauritius, Msumbiji, Namibia, Shelisheli, Swaziland, Tanzania, Zambia na Zimbabwe na Makao Makuu ya Jukwaa hili Kibunge yapo Windhoek, Namibia.

**Madhumuni ya kuanzishwa kwa Jukwaa la SADC – PF ni:-**

- (i) Kushawishi utekelezaji bora wa sera na mipango ya SADC ikiwa ni pamoja na itifaki na mambo mengine ya kisheria.
- (ii) Kushawishi misingi ya Haki za Binadamu, usawa wa Jinsia, na Demokrasia katika kanda ya SADC.
- (iii) Kuhakikisha uwepo wa amani, usalama na demokrasia kwa nchi wanachama.

- (iv) Kushawishi dhana nzima ya maisha bora ya sasa na yajayo kwa watu wa kanda hii ili hatimaye kwa pamoja waweze kujitegemea na kuwa na tija katika uchumi.
- (v) Kuratibu mawasiliano na Wabunge/Mabunge mengineyo ikiwa ni pamoja na asasi za Kitaifa na Kimataifa.
- (vi) Kutoa ushawishi kwa vyama visivyokuwa vya kiserikali, asasi na jamii za kisomi kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za SADC.
- (vii) Kuwepo kwa Jukwaa kwa ajili ya majadiliano kwa mambo yanayogusa hisia za nchi wanachama.
- (viii) Kuhakikisha uwepo wa utawala bora, uwazi na uwajibikaji katika kanda hii ya SADC na pia katika taasisi za SADC.
- (ix) Kuratibu uridhiwaji na utekelezwaji wa sera na sheria kwa nchi wanachama.
- (x) Kushawishi na kuwaelimisha wananchi wa nchi wanachama wa SADC kujua dhamira na madhumuni ya SADC.
- (xi) Hatimaye Jukwaa hili kuwa Bunge la Kanda ya SADC.

## **2. UWAKILISHI**

Kifungu cha 7 cha Katiba ya SADC PF kinaelekeza kuwa uanachama na muundo wa Jukwaa hili la Kibunge utakuwa na wawakilishi watano watakoachaguliwa na Bunge la Nchi Mwanachama. Kifungu hicho kinaelekeza kuwa katika mchakato wa kuwapata wawakilishi hawa kila Bunge la Taifa litahakikisha kuwa usawa wa kijinsia na uwakilishi wa vyama vya siasa Bungeni

unazingatiwa. Aidha, Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge wanawake (TWPG) anakuwa mjumbe kwa nafasi yake.

Mwakilishi kwenye Jukwaa hili la Kibunge atatumikia kuanzia tarehe aliyochaguliwa mpaka atakapokoma kuwa Mbunge au pale atakapoteuliwa kuwa Waziri au Naibu Waziri.

### **3. MUUNDO NA UANACHAMA WA SADC PF**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa mujibu wa Katiba ya SADC- PF, mwanachama wa SADC-PF ni Bunge lolote ambalo nchi yake ni mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika yaani SADC. Hivyo, muundo wa SADC PF ni mjumuiko wa Maspika (*Presiding Officers*) na Wabunge watano (5) waliochaguliwa kutoka kila Bunge la nchi mwanachama isipokuwa tu katika kuchagua Wabunge hao mambo yafuatayo yazingatiwe:

- (i) Kuhakikisha fursa sawa ya uwakilishi kwa wanawake na vyama vya siasa vyenye Wabunge.
- (ii) Katika nafasi hizo Tano (5) awepo Mwenyekiti wa chama cha Wabunge wanawake (*Women Parliamentarians Group*) ambaye ataingia kwa nafasi yake.
- (iii) Wanaochaguliwa kuwa Wawakilishi kwenye Jukwaa la Kibunge wasiwe na nafasi za Uwaziri.
- (iv) Wawakilishi hao wataliwakilisha Bunge lao katika SADC PF kwa kipindi cha miaka mitano (5) ya uhai wa Bunge.



SADC PF ina vyombo vinne vyenye majukumu mbalimbali ambavyo ni:-

**(i) Mkutano Mkuu wa Kibunge (*Plenary Assembly*)**

Chombo hiki kinajumuisha Maspika na Wabunge wawakilishi wa SADC PF waliochaguliwa toka Mabunge wanachama. Pamoja na majukumu mengine chombo hiki kazi yake kubwa ni kutunga sera pamoja na kutoa maamuzi kuhusu jambo lolote lililokubaliwa na wanachama.

**(ii) Kamati ya Utendaji (*Executive Committee*)**

Chombo hiki kinajumuisha Maspika na Wabunge (Ordinary Member) ambao huteuliwa na Spika kutoka miongoni mwa wawakilishi kwa mchanganuo ufuatao; Maspika saba (7) na Wabunge (Ordinary Member) saba. Wajumbe wa Kamati hii hudumu kwa kipindi cha miaka miwili (2).

Kazi kubwa ya Kamati ya Utendaji ni kusimamia maslahi ya wawakilishi wa SADC PF, kutoa mwongozo kwa Watumishi wa Sekretarieti ya SADC PF na kuhakikisha kuwa maamuzi yote yaliyofikiwa na Mkutano Mkuu yanatekelezwa.

**(iii) Ofisi ya Katibu Mkuu (*Office of the Secretary General*)**

Katibu Mkuu ambaye huidhinishwa na Mkutano Mkuu baada ya kupata mapendekezo toka Kamati ya Utendaji. Huidhinishwa kila baada ya miaka mitano (5).

Jukumu lake kubwa ni kuratibu shughuli zote za SADC-PF na kusimamia kazi za siku hadi siku za Jukwaa hili la Kibunge.

**(iv) Kamati za Kudumu za SADC PF (*Standing Committees*)**

Kwa mujibu wa Katiba ya SADC PF Mkutano Mkuu huunda Kamati za kudumu ili kurahisisha utendaji wa shughuli zake. Kamati hizo ni kama ifuatavyo;

- 1. Gender Equality, Women Advancement and Youth Development Committee*
- 2. Human and Social Development and Special Programs Committee*
- 3. Trade, Industry, Development and Integration Committee*
- 4. Food, Agriculture, Natural Resources and Infrastructure Committee*
- 5. Democratization, Governance and Human Rights committee*

Aidha, pamoja na kamati hizo kuna Umoja wa Kikanda wa Wabunge wanawake wa SADC (Regional Women Caucus).

**4. WAJUMBE WAWAKILISHI WA KWENYE SADC- PF**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa sasa Wajumbe wanaowakilisha Bunge letu la Tanzania katika SADC-PF pamoja na Kamati zao ni hawa wafuatao:-

- (i) **Mhe. Job Y. Ndugai, Mb**, Spika, na Rais wa Jukwaa la Kibunge la SADC
- (ii) **Mhe. Margaret S. Sitta, Mb**, Mjumbe, wa Kamati ya *Gender Equality, Women Advancement and Youth Development Committee*  
pia huwakilisha kwenye *Regional Women's Parliamentary Caucus (RWPC)* ya SADC-PF
- (iii) **Mhe. Selemani J. Zedi, Mb**, Mjumbe wa Kamati ya *Trade, Industry, Development and Integration Committee*
- (iv) **Mhe. Ally A. Saleh, Mb**, Mjumbe wa Kamati ya *Democratization, Governance and Human Rights committee*
- (v) **Esther M. Mmasi, Mb**, Mjumbe wa Kamati ya *Food, Agriculture, Natural Resources and Infrastructure Committee*
- (vi) **Mhe. Jamal K. Ali, Mb**, Mjumbe wa Kamati ya *Human and Social Development and Special Programs Committee*

## **5. SHUGHULI AMBAZO ZIMEFANYIKA KWA KIPINDI CHA JULAI – OKTOBA, 2016.**

Jukwaa hili la Kibunge hukutana mara mbili (2) kwa mwaka kwa mikutano yake ya Kibunge, pamoja na Mikutano hiyo, vikao vya kamati navyo hukutana mara mbili kwa mwaka. Mikutano ya Kibunge hufanyika kwa mzunguko kutoka miongoni mwa nchi

wanachama kwa kadiri wanavyojitolea kuwa mwenyeji wa mikutano hiyo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, pamoja na ratiba hiyo Kamati ya Utendaji nayo hukutano mara mbili (2) kwa mwaka. Aidha, Bunge huweza kushiriki shughuli mbalimbali ambazo husimamiwa na Jukwaa hili la Kibunge nje ya mikutano yake ambayo ipo kwa mujibu wa Katiba kwa kadiri fursa zinapopatikana.

Kwa mwaka huu wa fedha kuanzia Julai hadi Oktoba, 2016, Wawakilishi hawakuweza kushiriki kwenye shughuli za Jukwaa hili kutokana na changamoto zilizojitokeza ambazo zilikuwa nje ya uwezo wetu. Hata hivyo, Bunge lilishiriki katika zoezi la Ungalizi wa Uchaguzi Mkuu wa Zambia kuanzia tarehe 4 – 15 Agosti, 2016 kwa mwamvuli wa SADC PF na kuwakilishwa na Mhe. Restituta Mbogo, Mb, ambaye pia alichaguliwa kuwa *Mission Leader*.

## 6. CHANGAMOTO

Kutokuwa na mtiririko mzuri wa ushiriki wetu kunatokana na changamoto iliyopo sasa ya upatikanaji wa vibali vya safari. Kwani kwa sasa anayetoa vibali vya safari nje ya nchi ni Rais tu. Mfano wajumbe wamekosa kushirikiri vikao vya Kamati ambavyo vimefanyika tarehe 9 – 12 Oktoba, 2016 kutokana na kibali hicho kuchelewa kutoka.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa niaba ya Wawakilishi wenzangu naomba kutoa shukrani kwa utaratibu huu wa kuwasilisha taarifa kwa Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (2) (3), Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Huu

ni utaratibu mzuri unaowezesha Bunge letu kupitia Kamati hii kufahamu mambo mbalimbali yanayoamuliwa kikanda na kusimamia utekelezaji wake wa ndani ya nchi (*Domestication*). Mapendekezo yetu kuwe na utaratibu wa kuwakutanisha Wabunge wote kwa pamoja ili vyama hivi vya Kibunge viweze kueleza shughuli mbalimbali zinazofanywa na vyama ili kuwa na ufahamu wa pamoja.

Aidha, kwa ushauri tunaomba taarifa za vyama hivi vya Kibunge ziwe zinawasilishwa katika kipindi cha Kamati kuelekea Bunge la Bajeti Machi/Aprili kwani kwa kipindi hicho vyama vingi vinakuwa vimeshatekeleza majukumu yake mengi tangu kuanza kwa mwaka wa fedha.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa niaba ya Wawakilishi wa Bunge la Tanzania kwenye SADC PF naomba kuwasilisha.

Selemani J. Zedi, Mb

25 Oktoba, 2016

Kwa niaba ya Wajumbe wawakilishi

**TAARIFA YA WABUNGE WA TANZANIA KATIKA BUNGE LA JUMUIYA  
YA AFRIKA MASHARIKI KWA KIPINDI CHA JULAI, 2015 HADI JUNI,  
2016 ILIYOWASILISHWA KWENYE KAMATI YA MAMBO YA NJE  
ULINZI NA USALAMA TAREHE 29 AGOSTI, 2016**

---

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, hiki ni kikao cha kwanza baina ya kamati yako na Wawakilishi wa Tanzania kwenye Bunge la Afrika Mashariki. Kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu tunaoiwakilisha Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki (*East African Legislative Assembly – EALA*) napenda kukushukuru wewe binafsi na Kamati yako kwa kutenga muda wenu kuonana na sisi siku hii ya leo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, aidha, sisi Wabunge wa Tanzania katika Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (Bunge la JAM), tunakupongeza wewe binafsi na Wajumbe wa Kamati yako kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Spika kuwa wajumbe wa kamati hii muhimu. Tunapenda kuwaahidi kuwa tutashirikiana kwa karibu na kamati yako ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yaliyo mbele yetu.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, wafuatao ndio tunaoiwakilisha Tanzania katika Bunge la Tatu la JAM:

- |                                       |   |            |
|---------------------------------------|---|------------|
| 1. Mhe. Charles Makongoro Nyerere     | - | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Twaha Issa Taslima            | - | Katibu     |
| 3. Mhe. Dr. Nderakindo Perpetua Kessy | - | Mjumbe     |
| 4. Mhe. Adam Omar Kimbisa             | - | "          |
| 5. Mhe. Shy-Rose Saddrudin Bhanji     | - | "          |
| 6. Mhe. Angella Charles Kizigha       | - | "          |
| 7. Mhe. Abdullah Ally Mwinyi          | - | "          |
| 8. Mhe. Bernard Musomi Murunya        | - | "          |
| 9. Mhe. Maryam Yahya Ussi             | - | "          |

## 1.1 BUNGE LA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (BUNGE LA JAM)

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Bunge la JAM limeundwa chini ya Ibara ya 9 ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 1999, likiwa ni mojawapo ya Taasisi nane zilizo chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Bunge la Tatu la JAM lilianza tarehe 5 Juni, 2012 likiwa na jumla ya wabunge 45 wa kuchaguliwa kutoka nchi za Burundi, Kenya, Rwanda, Tanzania, na Uganda. Pamoja na wabunge wa kuchaguliwa wapo wabunge wengine saba wanaoingia kwa nafasi zao. Wabunge hao ni mawaziri wanaoshughulikia masuala ya Mtangamano kutoka katika kila Nchi mwanachama, Katibu Mkuu wa Jumuiya na Mwanasheria wa Jumuiya. Ukomo wa Bunge hili la Tatu utaishia Juni, 2017, baada ya uhai wake wa miaka mitano kumalizika.

Kama mnavyofahamu Spika wa Bunge la JAM huchaguliwa kwa mzunguko (on rotational basis) kutoka nchi wanachama kwa kipindi cha miaka mitano. Spika wa Bunge la Kwanza alikuwa ni Mhe. Abdulrahman Kinana kutoka Tanzania (Juni 2002 – Juni 2007); na Spika wa Bunge la Pili alikuwa ni Mhe. Abdirahim H. Abdi kutoka Kenya (Juni 2007 – Juni 2012). Spika wa tatu alikuwa mhe. Margaret Natongo Zziwa kutoka uganda (Juni 2012 hadi Desemba 2015). Spika wa sasa ni Mhe. Daniel F.Kidega kutoka Uganda.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Bunge la JAM linafanya shughuli zake kama zilivyoainishwa katika Ibara ya 49 (1), (2) na (3) ya Mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Bunge la JAM kama yalivyo Mabunge mengine, kazi zake kuu ni kutunga Sheria, kujadili na kupitisha Bajeti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na ni chombo cha Uwakilishi na kusimamia shughuli za Jumuiya.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Bunge la JAM kama yalivyo Mabunge mengi ya Jumuiya ya Madola, hufanya shughuli zake kupitia Kamati zake za Kudumu zinazoundwa chini ya ibara ya 49 (2) ya Mkataba wa JAM. Kwa hivi sasa Kamati hizo za Kudumu za Bunge la JAM ni:

1. Kamati ya Masuala ya kikanda na Usuluhishi(*Regional Affairs and Conflict Resolution Committee*);
2. Kamati ya Mawasiliano, Biashara na Uwekezaji (*Communications, Trade and Investment Committee*);
3. Kamati ya Masuala ya Jumla(*General Purpose Committee*);
4. Kamati ya kilimo, utalii na Mali Asili (*The Agriculture, Tourism and Natural Resources Committee*);
5. Kamati ya Sheria na Haki za Wabunge (*Legal Rules and Privileges Committee*) na
6. Kamati ya Hesabu (*Accounts Committee*).

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa hivi sasa Tanzania inashikilia uenyekiti wa Kamati ya Masuala ya kikanda na Usuluhishi ambapo Mwenyekiti wake ni Mhe. Abdullah Mwinyi. Aidha, Kwa utaratibu uliopo, Kila nchi inashikilia uenyekiti wa Kamati moja kwa mzunguko isipokuwa nchi moja hupata fursa ya kushika uenyekiti wa Kamati mbili. Hata hivyo wajumbe wa kamati hutoka katika orodha ya Wabunge wa Nchi Wanachama.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Bunge la Tatu la JAM kwa mara ya kwanza limeunda Tume ya Bunge (*Parliamentary Commission*), inayojumuisha Spika kama Mwenyekiti, Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri wa EAC na Wajumbe 2 wanao chaguliwa kutoka kila nchi Mwanachama. Kamati hii ndio hupanga na kuratibu shughuli zote za Mikutano ya Bunge la JAM na kuteua Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge hilo. Kwa kawaida wajumbe kamati hii hufanya kazi kwa kipindi cha miaka miwili na nusu. Kuanzia Juni 2012 hadi Desemba 2014 Tanzania iliwakilishwa na Mhe. Adam Kimbisa na Mhe. Shy-Rose Bhanji. Januari 2015 hadi Juni 2017 Tanzania inawakilishwa na Mhe. Charles Makongoro Nyerere na Mhe. Nderakindo Perpetua Kessy.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wabunge wa Tanzania wamegawanyika katika Kamati mbalimbali kama ifuatavyo:

1. *Regional Affairs and Conflict Resolution Committee*
  - Mhe. Abdullah A. Mwinyi- Mwenyekiti wa kamati
  - Mhe. Twaha I. Taslima
  - Mhe. Adam O. Kimbisa



2. *Communications, Trade and Investment Committee*

- Mhe. Angella C. Kizigha
- Mhe. Abdullah A. Mwinyi
- Mhe. Nderakiro P. Kessy

3. *General Purpose Committee*

- Mhe. Charles M. Nyerere
- Mhe. Angella C. Kizigha
- Mhe. Maryam Y. Ussi

4. *The Agriculture, Tourism and Natural Resources Committee*

- Mhe. Adam O. Kimbisa
- Mhe. Shy-Rose S. Bhanji
- Mhe. Bernad M. Murunya

5. *Legal Rules and Privileges Committee*

- Mhe. Twaha I. Taslima
- Mhe. Charles M. Nyerere
- Mhe. Maryam Y. Ussi

6. *Accounts Committee.*

- Mhe. Shy-Rose Bhanji
- Mhe. Nderakindo P. Kessy
- Mhe. Bernard M. Murunya

Aidha, Katika kipindi hicho Bunge lilifanya Mikutano Sita ambayo ilifanyika katika miji ifuatayo ya Nchi wanachama: Kampala, Nairobi, Kigali, Arusha, Dar es Salaam, Arusha.

## **2.0 MISWADA YA SHERIA ILIYOPITISHWA NA BUNGE**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika kipindi cha Mwaka 2015 na Juni 2016 Bunge la Afrika Mashariki lilipitisha Miswada kadhaa kama ifuatavyo:-

## **2.1 The East African Community Creative and Cultural Industries Bill, 2015**

Sheria hii inalenga kuinua ubunifu miongoni mwa nchi za Jumuiya ya Afirka Mashariki. Aidha, Sheria hii inaanzisha Baraza lenye jukumu la kuweka mazingira muafaka ya kuchochea ubunifu na uvumbuzi miongoni mwa Wananchi katika Jumuiya ya Afrika Mshariki. Vilevile Sheria hii inaanzisha Mfuko Maalumu (Fund) kwa ajili ya kusaidia miradi ya uvumbuzi na ubunifu miongoni mwa Wananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

## **2.2 The East African Community Electronic Transactions Bill, 2015**

Lengo la Sheria hii ni kurahisisha miamala ya Kieletronic kwenye mipaka ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Sheria hii inaweka mfumo wa Kisheria (legal framework) ili kuwezesha wawekezaji ndani ya Jumuiya kufanya miamala ya kieletronic bila vikwazo. Vilevile Sheria hii inaweka ulinzi (safeguards) dhidi ya matumizi mabaya ya usafirishaji wa fedha kwa njia ya kieletronic.

## **2.3 The East African Community Forests Management and rotection Bill, 2015**

Sheria hii inalenga kuweka hifadhi ya kisheria ya kikanda (regional framework) ili kulinda na kuhifadhi mazingira katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, lengo kuu la Sheria hii ni kuendeleza, kulinda na kusisitiza matumizi endelevu ya misitu katika ukanda wa Afrika Mashariki kwa ajili ya vizazi vilivyopo na vizazi vijavyo. Vilevile Sheria hii imeuhuisha Sheria za misitu miongoni mwa nchi Mwanachama.

## **2.4 The East African Community Disaster Risk Reduction and Management Bill, 2012**

Sheria hii inaweka mfumo wa Kisheria (legal framework) unaoziwezesha nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuchukua

hatua stahiki ili kujiandaa, kujilinda na kupunguza athari zinazosababishwa na majanga pale yanapotokea. Aidha, Sheria hii inalenga kuimarisha juhudi za kukabiliana na majanga na kutoa misaada kwa wahanga wa majanga ya asili hususan yale yanayotokana na mabadiliko ya tabia nchi.

## **2.5 The East African Community Customs Management (Amendment) Bill, 2016**

Sheria hii inalenga kuifanyia marekebisho Sheria ya Forodha ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2014 (The East African Customs Management Act, 2014). Lengo lake kubwa ni kuinua biashara kwenye ukanda wa Afrika Mashariki na kuhakikisha utekelezaji wa "Single Customs Territory" (SCT).

## **2.6 The East African Community Persons with Disability Bill, 2016**

Sheria hii inaweka ulinzi kamili (full protection) kwa watu wenye ulemavu ili kuwawezesha kunufaika na haki za msingi kama binadamu wengine. Kubwa zaidi Sheria hii inawawezesha watu wenye ulemavu kupata elimu na mafunzo stahiki kama nyenzo muhimu ya kuendeshea maisha yao. Vilevile Sheria hii inaweka mfumo stahiki wa Kisera, Kisheria, Kiutawala na Kibajeti ili kulinda haki na utu wa watu wenye ulemavu.

## **2.7 The East African Community Supplementary Appropriation Bill, 2016**

Sheria hii inaruhusu matumizi ya ziada ya fedha za Jumuiya kwenye bajeti yake ya mwaka 2015/2016.

## **2.8 The East African Community Appropriation Bill, 2016**

Sheria hii inatoa ridhaa kwa matumizi ya fedha za Jumuiya katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2016/2017

### 3.0 MAAZIMIO YA BUNGE

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika kipindi cha Juni, 2015 hadi Julai, 2016 Bunge lilijadili na kupitisha Maazimio kumi (10) kama ifuatavyo:-

- Azimio la Bunge la kumuenzi na kulaani mauaji ya Marehemu Hafsa Mossi aliyekuwa Mwakilishi wa Burundi kwenye Bunge la EALA. (Resolution of the Assembly to Condemn the killing of ,and to pay Tribute to the late Hon. Hafsa Mossi)
- Azimio la Bunge la kumuaga aliyekuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Mhe. Balozi Dr. Richard Sezibera. (Resolution of the Assembly to bid farewell to Hon. Amb. Dr Richard Sezibera outgoing Secretary General of the EAC)
- Azimio la Bunge la kuwashukuru wake wa Marais Waasisi wa Jumuiya(1967-1977).(Resolution of the Assembly to Thank the Founders and First ladies of the EAC (1967-1977)
- Azimio la Bunge la kuipongeza Nchi ya Jamhuri ya Sudan Kusini kwa kuwa Mwanachama wa EAC. (Resolution of the Assembly to Congratulate the Republic of South Sudan Admission into EAC)
- Azimio la Bunge la kumpongeza Mhe. Dr. John Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Resolution of the Assembly Congratulating the Fifth President of Tanzania, H.E. John Pombe Magufuli)
- Azimio la Bunge la kuzitaka Nchi za EAC kuridhia Itifaki Umoja wa nchi za Afrika (AU) kuhusu Bunge la Afrika lipate uhalali wa kuwa na mamlaka yote ya kibunge. (Resolution of the Assembly urging EAC Partner States to Ratify AU Protocol to the Constitutive Act of the African Union Relating to Pan African Parliament.)

- Azimio la Bunge la kuipongeza Nchi ya Uganda kwa kuwezesha upatikanaji wa vitambulisho(3rd Generation ID).(Resolution of the Assembly to Congratulate Uganda Upon Acquiring 3rd Generation National ID Cards)
- Azimio la Bunge la kutuma Salamu za rambirambi kwa Serikali ya Kenya kufuatia mauaji kwenye Chuo Kikuu cha Garissa. (Resolution of the Assembly to Condole the Government of Kenya over Tragic loss of lives in Garissa)
- Azimio la Bunge la kuzitaka Nchi za EAC kuridhia Mkataba wa Afrika kuhusu Demokrasia.(Resolution of the Assembly urging the EAC Partner states to Adopt the African Charter on Democracy)
- Azimio la Bunge la kuanzisha Kituo cha Kibunge cha Amani na Usalama kwa Nchi za Afrika Mashariki. (Resolution of the Assembly for the Establishment of EA Parliamentary Centre for Peace and Security.)

#### **4.0 TAARIFA ZA KAMATI ZA BUNGE**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika kipindi cha kati ya Februari na Julai 2016 Bunge lilijadili na kupitisha taarifa za kamati zake mbalimbali. Taarifa hizo ziliwasilishwa kwenye Mabunge ya Nchi wanachama kwa mujibu wa ibara ya 65 ya Mkataba wa EAC. Taarifa hizo ni kama ifuatavyo:-

- Report for an oversight activity on the security related challenges of implementing the Common Market Protocol along Central Corridor by the Committee on Affairs and Conflict Resolution.
- Report of the Committee on General Purpose on the EAC Annual (Financial) Report for the period 2013/2014.
- Report of the Committee on Legal, Rules and Privileges on the consideration of a resolution moved under rule 30 (j) of the

Assembly Rules of procedure on matter of privileges arising from a threat of tenure of office of four Members of EALA from the Republic of Burundi

- Report of the Committee on Regional Affairs and Conflict Resolution on the Public hearing on a petition by Pan African Lawyers Union (PALU) on the deteriorating Human Rights and humanitarian situation in Burundi;
- Report of the Committee on Accounts on the oversight activity undertaken with EAC Institutions on the Governance, project performance and implementation of the Assembly recommendations
- Report of the Committee on Legal, Rules and Privileges on the oversight activity on Harmonization of the National Laws in the EAC Context;
- Report of the East African Legislative Assembly on the sensitization activity conducted in Partner States in April and June, 2016.

## **5.0 MGOGORO WA BURUNDI**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kufuatia mgogoro wa Burundi kuendelea, Bunge kwa nafasi yake limeshiriki katika kutafuta suluhu ya mgogoro huo kwa kufanya mambo yafuatayo:

- i. Kamati ya Masuala ya Kikanda na Usuluhishi wa Migogoro ilifanya ziara katika Kambi za Wakimbizi zilizoko Kigoma na Rwanda. Pamoja na kuwa ziara hiyo ilifanyika katika kipindi cha mwaka 2014/15, Taarifa yake ilitolewa Bungeni katika kipindi hiki.

- ii. Kamati ilisikiliza pande zote muhimu katika mgogoro huo katika mkutano wa wazi (Public Hearing) uliofanyika Arusha. Pande zilizofika ni Serikali, Vyama vya Siasa na Wawakilishi wa Asasi za kiraia. Zoezi hilo lilifanyika kufuatia maombi (Petition) iliyoletwa Bungeni na Asasi za Kiraia.

## **6.0 MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA MGOGORO WA BURUNDI**

6.1 **Mheshimiwa Mwenyekiti**, kufuatia mgogoro unaoendelea Burundi, Waheshimiwa wabunge wanne (4) kutoka Burundi hawawezi kurudi nchini mwao kutokana na kuwa na msimamo tofauti na Serikali. Awali, Serikali ya Burundi iliwasilisha hoja ya kuwaondoa Ubunge wao katika Bunge la JAM. Hoja hiyo ilikataliwa na Bunge kwa sababu haikukidhi matakwa ya Mkataba wa Jumuiya na Sheria.

### **6.2 KUUAWA KWA MHE. HAFSA MOSSI.**

**Mheshimiwa mwenyekiti**, Tarehe 13 Julai, 2016 Mwakilishi wa Burundi kwenye Bunge la Afrika Mashariki Mhe. Hafsa Mossi aliuwawa. Bunge la Afrika Mashariki lilifanya kikao maalumu tarehe 22 Julai, 2016 mjini Arusha. Aidha, Bunge la Afrika Mashariki lilitoa Azimio la kulaani mauaji hayo tarehe 21 Julai 2016.

## **7.0 ZIARA YA WAKE WA MARAIS WA KWANZA WA TANZANIA, KENYA NA UGANDA.**

Mnamo tarehe 31 Mei, 2016, Bunge la Afrika Mashariki lilipata heshima ya kutembelewa na wake wa waliokuwa Marais na Waasisi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ya awali (1967 hadi 1977) ambao ni Mama Maria Nyerere, Mhe. Mama Miria Obote na Mhe. Mama Ngina Kenyatta huko Arusha. Mhe. Mama Maria Nyerere hakuweza kushiriki kwenye ziara hiyo kutokana na sababu za kiafaya. Katika ziara hiyo, Waheshimiwa Mama Miria Obote na Mama Ngina Kenyatta walipata fursa ya kulihutubia Bunge

la Afrika Mashariki. Hotuba zao zilielezea historia na kuisitiza umuhimu wa kuendeleza juhudi za kuleta Mtangamano wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

## 8.0 NANYUKI *SERIES* SEMINA (NANYUKI XI)

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Semina ya pamoja baina ya wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki na Mabunge ya Nchi Wanachama wa EAC ilifanyika Dar es salaam tarehe 3 hadi 4 Machi, 2016. Semina hii ni nyenzo mojawapo ambapo Bunge la Afrika Mashariki hukutana na mabunge ya Nchi wanachama kwa mujibu wa Ibara ya 49(2) ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lengo kubwa la semina hizi ni kuimarisha mahusiano na kutoa elimu na majadiliano juu ya masuala muhimu ya mtangamano baina ya Bunge la Afrika Mashariki na Mabunge ya Nchi Wanachama. Kauli mbiu ya semina ya X1 ilikuwa ni *Compliance with Regional and Sub regional Norms and Principles Governing Democratic Elections*. Semina hii ilifunguliwa rasmi na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bunge la Jamhuri ya Tanzania liliwakilishwa na Wenyeviti wa kamati za kudumu za Bunge wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama.

## 9.0 KUELIMISHA UMMA JUU YA MTANGAMANO WA AFRIKA MASHARIKI

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kama unavyofahamu, mojawapo ya jukumu la Bunge la Afrika Mashariki ni kuelimisha wananchi juu mtangamano wa Afrika Mashariki. Katika kipindi cha 2015/2016 tuliendelea kuelimisha umma kuhusu mtangamano wa Afrika Mashariki. Zoezi hilo lilifanyika katika awamu mbili kama ifuatavyo:

- i. **Awamu ya Kwanza:** Uhamasishaji ulifanyika kwa Kamati mbili za Bunge la Tanzania (Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na



Kamati ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji); Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam na Muhimbili pamoja na kutembelea vyombo vya habari vya TBC, ITV/Radio One, The Guardian, Mwananchi, Soko la Kariako na Soko la Samaki (Ferry), New Habari Corporation, City Radio FM, Clouds Radio na TV na Azam Media Group. Vilevile, uelimishaji ulifanyika kupitia mitandao mbalimbali ya kijamii.

- ii. **Awamu ya Pili:** Katika awamu ya pili Wabunge wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki walifanikiwa kukutana na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutoa elimu ya mtangamano na kukuza ufahamu juu ya shughuli na majukumu ya Bunge la Afrika Mashariki. Aidha tulikutana na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi walifurahishwa na hatua hiyo ya kutoa mrejesho na elimu juu ya shughuli za bunge la Afrika Mashariki na masuala ya mtangamano. Walitoa mwito wa zoezi hili kuwa endelevu.

Ziara yetu pia ilitufikisha Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Chuo Kikuu cha Mzumbe, CBE (Dodoma), Soko la Majengo (Dodoma), Umoja wa Wakulima wa Zabibu wa Chabuma AMCOS Ltd, (Chamwino), TCCIA- Morogoro, ZBC, Zenji FM na Zenj Digital Television, ZCCIA, Tume ya Utalii Zanzibar na Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA).

Tunapenda kurejea shukrani zetu kwa Uongozi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mhe. Job Yustino Ndugai(Mb) kwa kutupatia fursa adhimu ya kushauriana na waheshimiwa Wabunge wote Bungeni Dodoma mnamo tarehe 9 Juni, 2016.

Aidha, tunamshukuru Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama kwa kuendesha kikao hicho kwa ufanisi mkubwa. Ni dhahiri kuwa kutokana na muda

mfupi uliokuwepo hatukuweza kujibu maswali na hoja mbalimbali za Waheshimiwa wabunge kwa kikamilifu.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Programu ya kuelimisha wananchi kuhusu mtengamano wa Afrika Mashariki imedhihirisha kuwa wananchi walio wengi wana uelewa mdogo kuhusu fursa zitokanazo na mtangamano. Hivyo juhudi zaidi zinahitajika ili elimu hii iwafikie makundi mbalimbali ya wananchi hususan sekta binafsi mijini na vijijini.

## **10.0 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI JUMUIYA KWA SASA**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, sehemu kubwa ya changamoto nitakazoziainisha kwenye taarifa hii ni za muda mrefu. Wenzetu waliotangulia na sisi tuliopo tumewahi kuzizungumzia kwenye vikao mbalimbali baina ya Wizara na wadau wengine.

### **10.1 Nchi wanachama kutolipa Michango kwa wakati**

Jumuiya ya Afrika Mashariki inakabiliwa na Changamoto mbalimbali, lakini changamoto kubwa inayoikabili Jumuiya kwa sasa ni Nchi Wanachama kutokulipa michango yake na zile zinazolipa kuchelewa kufanya hivyo. Kulingana na Ripoti ya Mkutano wa Kamata ya Fedha na Utawala ya Jumuiya uliofanyika tarehe 10-12 Agosti 2016. Hali halisi ya madeni ya michango mpaka hivi sasa ni kama ifuatavyo:

PARTNER STATE	ARREARS (FY'15/16)	CONTRIBUTION DUE 2016/17	CONTRIBUTION PAID 2016/17		TOTAL OUTSTANDING
Republic of Kenya	-	8,378,108	330,306	3.94%	8,047,801
United Rep. of Tanzania	356,492	8,378,108	-	0.00%	8,734,599
Republic of Uganda	250,728	8,378,108	-	0.00%	8,628,836
Republic of Rwanda	-	8,378,108	-	0.00%	8,378,108
Republic of Burundi	5,609,800	8,378,108	-	0.00%	13,987,908
<b>Total</b>	<b>6,217,020</b>	<b>41,890,538</b>	<b>330,306</b>	<b>0.79%</b>	<b>47,777,252</b>

- 10.2 Wabunge wa Bunge la JAM kutoshirikishwa kikamilifu katika shughuli mbalimbali za kitaifa na kimataifa. Kwa mfano, ugeni wa kitaifa unaotembelea nchini au kunapokuwa na ziara za viongozi wakuu nje ya nchi huhusan zile za JAM, Wabunge wa Bunge ya JAM hatushirikishwi ipasavyo na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.
- 10.3 Kutokuwa na Sera ya Mtangamano wa JAM kunachangia baadhi ya shughuli kutotekelezeka kikamilifu. Tanzania bado hatuna Sera hiyo muhimu.
- 10.4 Changamoto nyingine inayotukabili ni kutokuwa na ofisi kwa ajili ya kutekeleza shughuli za kibunge tunapokuwa Dar es Salaam na Dodoma ( wabunge 8 kati ya 9 wanaishi Dar es Salaam. Aidha tunakutana Arusha mara mbili tu kwa mwaka kwa vikao vya Bunge). Kwa kipindi cha miaka minne tumekumbana na tatizo la kufanyia kazi nyumbani na mahotelini na vile vile kufanya vikao vyetu sisi wabunge kwa gharama zetu mahotelini. Hali hii inatuvunjia hadhi na haileti ufanisi.
- 10.5 Kwa kipindi cha miaka minne sasa, Wabunge wa Bunge la JAM tumeomba kupatiwa mikopo ya magari na Serikali kama ilivyo kwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini suala hili halijatekelezwa.

## 11.0 MAONI NA USHAURI


- 11.1 Kwa kuwa kumekuwa na matukio mengi ya Kitaifa na Kimataifa, ambayo Wabunge wa Bunge la JAM tumekuwa hatushirikishwi ipasavyo; tunaomba Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kutushirikisha Wabunge wa Bunge la JAM kwa kualikwa kuhudhuria matukio ya kitaifa na vile vile kupata mialiko pale ambapo viongozi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na wale wa Kimataifa wanapokuwa katika ziara za kikazi hapa nchini;
- 11.2 Aidha, tunaishauri Serikali itenge fungu maalumu ili kuwawezesha Wabunge wa EALA kufanya ziara nchi nzima kwa lengo la kuelimisha Wananchi kuhusu fursa zitokanazo na Mtangamano wa Afrika Mashariki
- 11.3 Tunashauri pia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki iandae Semina kwa Waheshimiwa Wabunge wote ili kutoa elimu ya Mtangamano na masuala mbalimbali ya Bunge la Afrika Mashariki na Jumuiya kwa ujumla.
- 11.4 Kwa kuwa Wabunge wa JAM kwa muda mrefu tumekuwa tukitumia fedha zetu katika kutekeleza majukumu ya uwakilishi, Serikali iangalie namna ya kutuwezesha kwa kupatia ofisi, pamoja na vitendea kazi kama vile *computer, printer, scanner, fax*, simu n.k;
- 11.5 **Mheshimiwa Mwenyekiti**, tunaomba uangaliwe uwezekano wa kutupatia usafiri sisi Wabunge 9 wa Tanzania kuweza kutumia katika shughuli zetu za kibunge pindi tukiwa Arusha, Dar es Salaam na Dodoma na kupitia shughuli zetu za uhamasishaji kwa shughuli za Jumuiya.
- 11.6 **Mheshimiwa Mwenyekiti**, tumekwisha fanya safari kadhaa katika maeneo tuliyoyataja ikiwemo kwenda Dodoma tunapo hudhuria vikao vya Bunge wakati Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki inapowasilisha Bajeti yake (2012/2013 na 2013/2014). Safari zote zimefanyika katika mazingira magumu.

11.7 **Mheshimiwa Mwenyekiti**, baadhi yetu Wabunge wa JAM tumekopa magari ili kujisitiri na adha ya usafiri, jambo ambalo hupelekea kukatwa fedha nyingi kutoka katika mishahara yetu ya mwisho wa mwezi ili kufidia madeni hasa ukizingatia mshahara tunaoupata bado ni mdogo sana. Tunapendekeza au Serikali itupatie magari, ambayo tutayarudisha baada ya kipindi chetu cha uchaguzi au tupewe *grant* ya asilimia 50.

#### 11.10 **HITIMISHO**

Mhe. Mwenyekiti kwa niaba ya Wahe. Wabunge wenzangu napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa dhati kwa mwaliko huu wa kutufikisha hapa Dodoma kwa ajili tya kuwasilisha ripoti yetu ya mwaka na kubadilishana mawazo. Tuko tayari kuitikia wito kila itapohitajiwa kufanya hivyo.

Naomba kuwasilisha.

  
Mhe. Charles Makongoro Nyerere (Mb)  
**MWENYEKITI**  
**WABUNGE WA TANZANIA – EALA**  
Septemba, 2016